Nipashe
Jumatatu Oktoba 19, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580373
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



**MWINYI** ahakikishia diaspora ushirikiano UKURASA 3



**MWENYEKITI** atupwa miezi sita jela kwa wizi UKURASA 4

**Solskjaer: Sasa Utd imeanza ligi rasmi** UKURASA 22

UCHAGUZI 2020

# Siku 9 za lala salama

• **CCM**, CHADEMA kutimua vumbi Kaskazini... *Endelea ukurasa 2*





## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**WALIOKIMBIA MAPIGANO MSUMBIJI WAKAMATWA, WARUDISHWA KWAO**

UKURASA WA 5
**QUALITY GROUP YAAMRIWA KULIPA WAANDISHI MIL. 230/-**

## 57 mbaroni tuhuma za kujeruhi watano Pemba

UKURASA 2



Rais, Dk. John Magufuli, akimkabidhi mfano wa funguo Rais wa Awamu ya Pili, Alhaj Ali Hassan Mwinyi na mkewe, Mama Sitti Mwinyi, katika hafla ndogo ya kumkabidhi nyumba ambayo serikali imemjengea Mzee Mwinyi kwa mujibu wa sheria, eneo la Masaki jijini Dar es salaam jana. **Habari Uk. 3**. **PICHA: IKULU**

## Lissu aitaka NEC kutenda haki kwa mawakala wote

UK. 2

Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

**Fursa kwa Wagombea! 2020**
VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini
Je ungependa kukishukuru chama chako ?
Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?
Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz
VOTE

HABARI KITAIFA



Mgombea wa Urais kupitia CHADEMA, Tundu Lissu, akihutubia mkutano wa kampeni katika viwanja vya Raha, Wilaya ya Babati, mkoani Manyara jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tundu Lissu ataka NEC kutendea haki mawakala vyama vyote

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA urais wa jamhuri ya Muungano kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA), Tundu Lissu, ameiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutenda haki kwa mawakala wa vyama vyote vinavyoshiriki katika uchaguzi.

Akiwa katika mikutano yake mjini Babati mkoani Manyara, Lissu, alisema ni vema NEC ikahakikisha kwamba mawakala wa vyama vyote wanaapishwa, wanapewa barua za utambulisho na wanapatiwa nakala na matokeo katika kila kituo bila kisingizio chochote.

Lissu alisema kufanya hivyo kutachangia uchaguzi huo kuwa huru na wa haki.

Lissu alisema ni haki kisheria kila chama kuwa na wakala katika kila kituo cha uchaguzi na si fadhila.

"NEC imeweka kanuni inayosema kwamba wakala akishaapishwa anapewa barua ya utambulisho na anaenda nayo kituoni, mwaka huu imesema kwamba hiyo barua ya utambulisho itapelekwa na msimamizi wa uchaguzi kwenye vituo sahihi," alisema na kuongeza:

"Sasa hii inaweza kuleta shida kwa sababu wakala anaweza akafika kwenye kituo na msimamizi akamkataa kwamba hana jina lake katika kituo hicho, akamwambia akatafute kituo kingine."

"Kwa hiyo badala ya wakala kupaswa kuwa katika kituo cha shule ya msingi Mbangwa, barua yake ya utambulisho inapelekwa Kateshi, sasa mpaka uje uipate tayari saa kumi jioni imefika, sheria inasema tuna haki ya kuwa na mawakala katika vituo na siyo fadhila. Kwa hiyo tunachoomba sisi ni NEC kuhakikisha inawapatia barua za utambulisho mawakala wote katika kila kituo." Aidha, Lissu aliiomba NEC kuhakikisha inakuwa na nakala za kutosha za matokeo ya kila kituo kwa ajili ya kuwapatia mawakala.

"NEC wahakikishe kwamba kila wakala anapatiwa nakala ya matokeo, wakala asipopewa nakala maana yake anakosa ushahidi wa kura katika kituo, na ni haki yake kupatiwa," alisema Lissu. "Tume ya uchaguzi, watendaji na wasimamizi wa uchaguzi, wana wajibu wa kuwaapisha mawakala, wakikataa kwa kisingizio chochote wanataka kuharibu, sheria inasema tuwe na mawakala."

Tayari zimebaki siku tisa kabla ya kufikia siku ya uchaguzi mkuu, Oktoba 28, Watanzania kuchagua rais, wabunge na madiwani.

# Ni Siku 9 za lala salama uchaguzi 2020

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimesalia siku tisa kuelekea Oktoba 28, siku ya kupiga kura nchini, wagombea urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, wameonekana kumalizia ngwe ya kampeni zao mikoa ya Kanda ya Kaskazini, kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kuiongoza Tanzania.

Kila mgombea kwa sasa anafanya ushawishi wa mwisho na kukamilisha ratiba ya kampeni huku baadhi ya vyama vikionyesha kufunga kampeni zake mikoa iliyozindulia.

Licha ya vyama 16 kusimamisha wagombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini wagombea wa vyama viwili, CCM na CHADEMA, ndiyo wameonekana kutikisa kampeni za urais kwa upande wa Tanzania Bara.

Wagombea wa vyama vingine wanaofuatia ni wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba huku mgombea wa ACT-Wazalendo, Bernard Membe, akiwa kimya na kutoonekana katika majukwaa ya kampeni za kisiasa, baada ya Kiongozi Mkuu wa chama hicho, kutangaza kumuunga mkono mgombea urais kwa tiketi ya CHADEMA.

Mwingine ni wa chama ADC, Queen Sendiga, anaonekana maeneo mbalimbali nchini kwenye mikutano ya hadhara ya kampeni kuomba ridhaa ya kuwa rais wa awamu ya sita.

Kwa mujibu wa ratiba, wagombea urais upande wa Tanzania Bara, Lissu na Dk. Magufuli wanaonekana kuelekeza nguvu zao mikoa ya Kanda ya Kaskazini na Kati, ambako baadhi ya maeneo watakuwa wakipishana.

Ratiba ya kampeni ya siku tisa zilizosalia iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), CCM imeonyesha kuwa kwa sasa inaelekea mikoa ya Kaskazini yaani Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Aidha, mgombea wa chama hicho anatarajia kufunga kampeni zake mkoa aliozindulia, Dodoma, Oktoba 27.

Juzi, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Hamphrey Polepole, aliwaeleza waandishi wa habari kuwa mgombea wao ataanza ngwe ya mwisho ya kampeni zake katika mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na atamalizia Dodoma.

Alisema leo Dk. Magufuli atakuwa mkoani Pwani na atakwenda hadi Tanga, na baadaye kumaliza Kaskazini kabla ya kufunga kampeni zake jijini Dodoma, ambako ndiko alikozindua kampeni zake. Kwa upande wa ratiba ya mgombea urais kwa tiketi ya CHADEMA, Lissu, mikutano yake inaonyesha atarudi kwa mara ya pili hasa maeneo alikozaliwa Ikungi, mkoani Singida.

Ratiba hiyo ilionyesha kuwa, juzi alifanya mikutano katika Wilaya za Manyoni, Bahi, Kongwa na Dodoma mjini.

Jana alifanya mikutano katika wilaya za Hanang, Mbulu na Karatu.

Leo, atafanya mikutano sita katika wilaya za Simanjiro, Monduli, Longodi, Arumeru, Hai na Moshi mjini.

Oktoba 20, atafanya mikutano Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro na Lushoto mkoani Tanga, na siku inayofuata atashambulia maeneo ya Korogwe, Muheza na Tanga mjini ambako mgombea wa CCM atakuwa ameshamwaga sera zake.

Pia, Lissu atakwenda mikoa ya Kusini Oktoba 23 na atafanya mikutano Lindi, Nachingwea, Newala na Nanyumbu na Oktoba 24, atakuwa maeneo ya Tunduru, Nyasa na Songea mjini.

Pia, atarudi tena mkoa alikozaliwa na kufanya mikutano katika maeneo ya Chemba, Singida na Ikungi.

Oktoba 26, atarudi Kanda ya Kaskazini mikoa ya Kilimanjaro na Tanga na kufanya mikutano maeneo ya Same, Handeni na Pangani.

Anatarajiwa kufunga kampeni zake jijini Dar es Salaam, ambako ndiko alikozindua kampeni zake.

Kwa mujibu wa ratiba ya NEC, vyama vya ADC, CUF, CHAUMMA na UMD vitafungia kampeni zao jijini Dar es Salaam, huku vyama vya AAFP na DP vikimalizia Songwe. Vyama vingine na maeneo vitakapomalizia kampeni zao kwenye mabano ni ACT-Wazalendo (Lindi), ADA TADEA (Simiyu), Demokrasia Makini (Iringa), NCCR-Mageuzi (Mara), NRA (Tanga) na UPDP (Mbeya).

NEC ilitangaza kuwapo na vituo vya kupigia kura 80,155 huku waliojiandikisha ni 29,188,347 ambao watachagua wabunge 390 na madiwani 5,350.

Kampeni za uchaguzi zilipangwa kufanyika kwa siku 64, huku kila mgombea akitoa ahadi ya kuleta mabadiliko au kuendeleza yaliyofanyika.

# 57 washikiliwa tuhuma kujeruhi watano Pemba

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

WATU 57 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa Kaskazini Pemba, kutokana na vurugu baina ya wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT-Wazalendo katika Kijiji cha Kwale Shehia ya Majenzi Micheweni.

Kwa mujibu wa tarifa ya Kamanda wa Polisi mkoa Kaskazini Pemba, Juma Sadi, watuhumiwa waliwakamata kijijini humo na kwamba wanahojiwa na uchunguzi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Aidha, alisema msako unaendelea kwa watu wengine na kwamba wanaume wamehama makazi hao na kubaki wanawake na watoto. "Tunadhani wamekimbilia Tanga au Mombasa kwani hapa Pemba tumewasaka kila kona ya maeneo hatuja waona ila tutawashika wote tuwapeleke mahakamani," alisema.

Watu hao walikamatwa kwa madai ya kuwajeruhi vibaya watu watano ambao ni Khamis Hamad Haji (70), Yasiri Hemed Abdi (18), Abdalla Khamis Mbarouk (30), Juma khatibu Khatib Rajabu (36) na Hsasan Khamis Hamad (23) ambao walijeruhiwa na vitu vyenye ncha kali na wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Micheweni.

Alisema upelelezi utakapokamilika watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yatakayowakabili.

Daktari wa zamu katika hospitali hiyo, Dk.Yahaya Faki Khamis, alisema aliwapokea majeruhi hao na kuwapatia matibabu akiwamo Khatibu Saidi Khatibu aliyekatwa na kitu chenye ncha kali kwenye utumbo.

# Magufuli amkabidhi nyumba Mzee Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, jana alimkabidhi nyumba mpya ya kuishi Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi iliyopo Masaki jijini Dar es Salaam.

Nyumba hiyo imejengwa na Serikali ya Tanzania na kisha kukabidhiwa kwa Mhe. Rais Mstaafu Mwinyi kwa mujibu wa sheria ya mafao ya viongozi wa kisiasa namba 3 ya mwaka 1999 na marekebisho yake ya mwaka 2005 ambayo inaelekeza kuwa Marais wanapostaafu wanastahili kujengewa nyumba na Serikali.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurian Ndumbaro, alisema ujenzi wa nyumba ya Rais Mstaafu Mwinyi ulioanza mwaka 2005 ulisimama kwa muda mrefu na baadaye mwaka 2018 uliendelea chini ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kupitia Shirika lake la Suma JKT kwa ushirikiano na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) hadi ulipokamilika.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa nyumba hiyo, Rais Mstaafu Mwinyi alimshukuru Mhe. Rais Magufuli kwa kutoa msukumo mkubwa wa kukamilishwa kwa nyumba hiyo na pia ameishukuru Suma JKT na TBA kwa kujenga kwa ubora wa hali ya juu.

Rais Magufuli alimpongeza Rais Mstaafu Mwinyi kwa kupata nyumba hiyo, na amemtakia heri na maisha mema katika makazi yake hayo mapya. Pia ameipongeza Suma JKT na TBA kwa kukamilisha ujenzi wa nyumba hiyo.

Wakati huo huo, Mhe. Rais Magufuli amekagua jengo la nyumba ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete inayojengwa katika eneo la Kawe Jijini Dar es Salaam. Ujenzi wa nyumba hiyo ulianza mwaka 2018 chini ya TBA na Rais Magufuli ameiagiza TBA kuhakikisha ujenzi wa nyumba, uzio na mandhali yake unakamilika ifikapo tarehe 30 Januari, 2021. Aidha, Rais Magufuli ameiagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kujenga barabara ya lami yenye urefu wa meta 800 itakayounganisha nyumba hiyo na barabara ya lami iliyokaribu nayo.

Rais Mstaafu Kikwete alimshukuru Rais Magufuli kwa ujenzi wa nyumba hiyo ambayo amesema anatarajia ndipo ataishi maisha yake yote.

Mapema jana subuhi, Rais Magufuli akiwa na Mkewe Mama Janeth Magufuli walikwenda kumsalimu Mjane wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mama Anna Mkapa nyumbani kwake Masaki Jijini



Mwanafunzi Erick Rogers wa Shule ya Sekondari Tanga Ufundi ( TTS) akimuonesha Waziri wa Afya , Maendeleo ya Jamii , Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, namna walivyobuni mfumo wa uzalishaji umeme wakati wa maonesho ya Sayansi yaliyofanyika jana shuleni hapo. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Mwinyi ahakikishia diaspora ushirikiano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema wanaoishi nje ya nchi (Diaspora), wana mchango mkubwa wa kusaidia uchumi wa nchi kwa kuwekeza nchini ili Taznania ikiwamo Zanzibar kupata maendeleo.

Aliyasema hayo Mjini Zanzibar wakati akizungumza na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi ikiwa ni muendelezo wa kampeni zake na kukutana na makundi ya watu mbalimbali.

Alisema endapo atapata ridhaa ya kuiongoza Zanzibar, anakusudia kufanya mapinduzi katika kukuza uchumi kwa kushirikiana na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Alisema iwapo ataingia madarakani, atahakikisha anaweka mazingira mazuri kwa diaspora kuona wanaendelea kusaidia maendeleo ya nchi yao.

Dk. Mwinyi, aliwapongeza kwa utayari wao katika kuwasaidia Wazanzibari wenzao ambayo ndio azma ya serikali kushirikisha watu mbalimbali waliopo katika nchi mbalimbali kusaidia nchi yao.

"Azma yetu ya Chama Cha Mapinduzi katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi, kundi lenu tunalihitaji sana katika hili ikiwamo kupata wataalamu wazalendo ambao mtasaidia kukuza uchumi wetu kupitia sekta mbalimbali hasa uchumi wa bahari kuu," alisema.

Dk. Mwinyi aliwahakikishia Wazanzibari nje ya nchi ambao wapo tayari kurudi nyumbani, Serikali ipo tayari kuwatumia katika utaalamu wao katika sekta mbalimbali.

Hata hivyo, alisema anatambua juhudi zinazochukuliwa na serikali ya awamu ya saba kwa kutengeneza sera na sheria ya diaspora, na kuahidi atakapoingia madarakani ataaza kutekelezwa mara moja.

Aliahidi kulinda maslahi ya diaspora kwa kile wanachokiwekeza na kupata haki zao kama wazawa.

Aliwaomba kuendelea kutoa misaada katika nchi yao na kufikiria kufanya makubwa zaidi hasa kuimarisha huduma mbalimbali za kitaalamu.

"Tunataka kuwa na hospitali ya rufani ambayo itakuwa na wataalamu mbalimbali, hatutaki kuona mgonjwa wa moyo anapelekwa sehemu nyingine, lengo letu atibiwe hapa hapa kama wanavyofanya wenzetu Tanzania bara kwa Hospitali ya Jakaya Kikwete," alieleza.

Alisema katika kufanikisha hilo, ni jukumu la serikali kuona inaweka mazingira mazuri ikiwamo vifaa tiba na mambo mengine muhimu.

Naye, Mkurugenzi wa Idara ya ushirikiano na uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, Adila Hilal Vuai, alisema lengo la diaspora ni kushirikiana katika maendeleo ya nchi yao ikiwa ni dhamira ya serikali ya awamu ya saba chini ya Dk. Ali Mohamed Shein.

Alisema, wapo Wazanzibari wanaoishi nchi mbalimbali zikiwamo Denmamk, Oman, Uk, Jaman, Ethiopia, China, Canada na nchi nyengine, ambao ni wachangiaji wakubwa katika nchi yao kupitia sekta mbalimbali zikiwemo elimu na afya.

Kwa upande wao, Diaspora walisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kutokubalika kumiliki ardhi kwa kisingizio sio wazawa na kutotambulika na masheha katika maeneo wanayoishi wakiwa Zanzibar.


IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

Probate and Administration Cause No. 56 of 2020

In the matter of the estate of the late MONICA YARED MAMBO
Of Ntyuka within Dodoma City

And

In the matter of application for letters of administration by ALPHA MHINA MAMBO

**GENERAL CITATION**

(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 20 day of 10...2020

Dated at Dodoma this 1 day of 10.....2020.

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA REGION



KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU INVESTMENT COMPANY LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 796 BQQ** AINA YA **SUNLG** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **MAS/RB/8015/2020.**



**Procurement Opportunities**

Tender for Framework Agreements

Medical Teams International is Non-Government Organization (NGO) which was founded in 1979, providing life-saving medical care for people in crisis, such as survivors of natural disasters and refugees.

Medical Teams International, Kasulu Tanzania is inviting interested suppliers to express their interest to supply MTI with items per description below. All interested parties are invited to participate.

| | |
|---|---|
| **Procuring Entity:** | Medical Teams International |
| **Tender No:** | MTI20/GEN PROC/001 |
| **Tender Name** | Invitation to Tender for Framework Agreements |
| **Reference Number** | **CATEGORY A: SUPPLY OF GOODS** |
| PP/MTI-TAN/01/2020 | Supply of general stationery. |
| PP/MTI-TAN/02/2020 | Supply of office supplies. |
| PP/MTI-TAN/03/2020 | Supply and maintenance of photocopiers, scanners, computers, printers, Uninterruptible Power Supply (UPS), laptops, software, toners and other ICT accessories. |
| PP/MTI-TAN/04/2020 | Supply of branded items and promotional materials. |
| PP/MTI-TAN/05/2020 | Supply, installation and maintenance of fire and security alarms equipment and security systems. |
| PP/MTI-TAN/06/2020 | Supply of Fuel (Diesel & Petrol) |
| PP/MTI-TAN/07/2020 | Supply of bottled water, dispensing machines and maintenance. |
| PP/MTI-TAN/08/2020 | Supply of motor vehicle/cycle parts and accessories. |
| PP/MTI-TAN/09/2020 | Supply of airtime and scratch cards. |
| PP/MTI-TAN/010/2020 | Supply of office furniture's and fixtures. |
| PP/MTI-TAN/011/2020 | Medicines |
| PP/MTI-TAN/012/2020 | Medical Consumables |
| PP/MTI-TAN/013/2020 | Medical Equipments |
| **Reference Number** | **CATEGORY B: PROVISION OF SERVICES** |
| PP/MTI-TAN/014/2020 | Provision of catering services. |
| PP/MTI-TAN/015/2020 | Provision of air travel, reservations and ticketing services. |
| PP/MTI-TAN/016/2020 | Provision of sanitary, fumigation, pest control and cleaning services. |
| PP/MTI-TAN/017/2020 | Provision of internet services. |
| PP/MTI-TAN/018/2020 | Provision of hotel accommodation and conference facilities. |
| PP/MTI-TAN/019/2020 | Provision of security services (guards, dog patrols and security survey). |
| PP/MTI-TAN/020/2020 | Servicing, repair and maintenance of vehicles and motorcycles |
| PP/MTI-TAN/021/2020 | Vehicle Hire-minibus, pickups, hardtop Landcruiser's |
| PP/MTI-TAN/022/2020 | Provision of printing services |
| **Source of Fund** | Bureau of Population, Refugees and Migration & UNHCR |
| **Eligible Firms** | National (Registered in Tanzania) |
| **Method of Procurement** | National Competitive Bidding |
| **Mode Application** | Via Email; procurementtz@medicalteams.org (Please send an introduction email for document inquiry) |
| **Deadline** | 11th November 2020 4:30PM |
| **Bids Submission** | Effective 12rd October to 11th November 2020 |

*"Daring to love like Jesus, we boldly break barriers to health and restore wholeness in a hurting world"*

215940502

## Waliokimbia mapigano Msumbiji wakamatwa, warudishwa kwao

**Na Said Hamdani,** LINDI

RAIA 18 wakiwamo wanawake saba na watoto kutoka Msumbiji walioingia nchini bila ya kufuata sheria na taratibu za Idara ya Uhamiaji kwa madai ya kukimbia mapigano, wamekamatwa na kurejeshwa kwao.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, ACP Stanley Kulyamo, wahamiaji hao walikamatwa na askari polisi Oktoba 3, mwaka huu, mtaa wa Kineng'ene, Manispaa ya Lindi.

Alisema askari hao waliokuwa wakitekeleza majukumu yao, waliwakamata wahamiaji hao na baada ya mahojiano wakakabidhiwa Idara ya Uhamiaji kwa hatua zingine za kisheria ikiwamo kuwarejesha makwao.

Aliwataja wakimbizi hao kutoka Jimbo la Kabrigado kuwa ni, Mussa Anga, Hadija Rajabu, Robert Damiani, Josephine Damiani, Tito Thomas, Brayson Tito, Zamina Tito na Florence Thomas.

Wengine ni Fadina Mussa, Rehema Mussa, Esha Mussa, Amina Mussa, Agnes Philipo, Mashaka Philipo, Mariamu Said, Mohamedi Mussa na Benifesia Mkapa. Alisema kukamatwa kwa raia hao kumetokana na kuingia nchini kupitia njia zisizokuwa rasmi na kuishi bila ya kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na mamlaka zikiwamo kutokuwa na vibali vinavyowaruhusu kufanya hivyo.

Pia, Kamanda aliitaka jamii kutokumbatia wageni badala yake wafuate taratibu kwa kutoa taarifa kwa vyombo vya dola.

## TAKUKURU Pwani yachunguza tuhuma tisa rushwa uchaguzi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

OFISI ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Pwani, imesema kwasasa inashughulikia tuhuma tisa za rushwa ya uchaguzi zilizoripotiwa katika ofisi za wilaya mkoani hapo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akitoa taarifa ya utendaji kazi wa Taasisi hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu.

Suzana alisema, kesi hizo zipo na kwasasa zinaendelea kufanyiwa kazi na uchunguzi ukikamilika sheria itachukua mkondo wake.

Alisema kesi hizo zimeripotiwa katika ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Rufiji, Kibiti, Chalinze na katika ofisi ya mkoa.

Akizungumzia taarifa za rushwa ya ngono, alisema zipo ambazo zimeanza kuripotiwa mwezi huu na zimeanza kufanyiwa kazi.

"Taarifa za rushwa ya ngono zipo ila tunakosa ushahidi kwa kuwa wanaotoa taarifa hawatupi ushirikiano wakati wa uchunguzi," alisema Suzana.

Alisisitiza wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kuwa vipo vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuthibitisha.



Mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia chama cha Alliance For Democratic Change (ADC), Queen Sendiga, akigawa vipeperushi vyake kwa wafanyabiashara wa soko la mashine tatu mjini Iringa juzi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Sendiga kumpa JPM uwaziri

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MGOMBEA urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), Queen Sendiga, amesema akichaguliwa kuwa Rais wa Tanzania, akiunda baraza la mawaziri atampa nafasi Rais John Magufuli, kuwa waziri wa ujenzi.

Aidha, baada ya kuapishwa atafanya maboresho makubwa katika sekta ya afya kwa huduma za ngazi za chini kuboreshwa kwa kuwa na zahanati za kisasa kila kijiji.

Akiomba kura kwa wananchi wa Iringa mjini jana, alisema mtu pekee mwenye uwezo wa kusimamia sekta ya ujenzi ni mgombea Dk. Magufuli kutokana na kuimudu vyema sekta hiyo alivyokuwa Waziri katika serikali zilizopita.

Alisema pia atahakikisha wagombea urais wote walijitokeza kuwania nafasi hizo wanapata nafasi za uongozi ndani ya serikali yake kulingana na sifa na uwezi wao.

Sendiga alisema ameamua hivyo kutokana na ukweli kuwa chama chake hakina wagombea ubunge wa kutosha nchini na kwamba itakuwa vigumu kupata mawaziri wa kutosha ndiyo maana lazima achukue wagombea urais ambao tayari wameonesha uwezo wao. Alisema kuwa katika mchakato wa kampeni unaoendelea mbali ya kufanikiwa kupita mikoa zaidi ya 15 hadi sasa, ila amefuatilia kampeni za wagombea wenzake na sera zao na sehemu kubwa anajua ni yupi atamchukua katika serikali yake kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. Kwa mujibu wa mgombea huyo, bado kuna changamoto kubwa katika uboreshaji wa sekta ya afya kwa kuwa na zanahati kila kijiji kwake ni kipaumbele maana wananchi wanapata kero kubwa sana ya huduma za afya vijijini na uboreshaji huo utakwenda sambamba na vifaa tiba zikiwemo dawa.

Alisema kuwa hali ya uchumi siyo nzuri miongoni mwa Watanzania pamoja na serikali kujinasibu kuwa uchumi umekua ila uchumi huo hauwalengi moja kwa moja wananchi kuwa na fedha katika mifuko yao ambapo ADC watahakikisha wanatumia rasilimali zilizopo kukuza uchumi.

"Jukumu lingine kubwa kwa Serikali makini inayojali maisha ya watu ni kupanga namna njema ya matumizi ya rasilimali zilizopo kwenye maeneo husika kwa manufaa ya wakazi wake.

Aidha, alisema akiwa raia atarejesha ujenzi wa kiwanda cha gesi Mtwara kama namna ya kurejesha matumaini kwa wananchi wa kusini na kwamba serikali yake haitawakopa mazao wananchi na badala yake itawatengenezea mfumo wa kuwalipa kabla ya kuchukua mazao yao.

# Mwenyekiti jela miezi sita kwa wizi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mwanzo Mtama, Mkoa wa Lindi, imemhukumu Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Narwadi, Hassani Mtambo (35), kulipa faini ya Sh. 300,000 au kwenda gerezani miezi sita kwa kosa la kuiba na kukutwa na mali za mradi wa maji.

Hukumu hiyo ilitolewa Oktoba 16, mwaka huu na Hakimu wa mahakama hiyo, Edwin Rutalemba, baada ya mshtakiwa kukiri kosa.

Kabla ya hukumu hiyo, mshtakiwa ambaye pia ni mlinzi wa mali hiyo, aliulizwa kama ana sababu za msingi ili mahakama isimpe adhabu kali kwa kosa linalomkabili na kujitetea kuwa na familia inayomtegemea, hivyo akipewa adhabu kali kutaifanya ikose huduma zake. Baada ya utetezi huo, Hakimu Rutalemba, alimhukumu kulipa faini ya Sh. 300,000 na iwapo atashindwa atumikie kifungo cha miezi sita gerezani. Hata hivyo, mshtakiwa ameshindwa kulipa faini hiyo na kwenda kutumikia kifungo hicho gerezani.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mshtakiwa ambaye pia ni kiongozi wa Serikali ya Kijiji cha Narwadi, huku akiwa amechukuwa jukumu la ulinzi wa kulinda vifaa vya mradi huo, aliiba mifuko 19 ya saruji pamoja na nondo 11, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. 500,000.

HABARI KITAIFA

# Quality Group yaamriwa kulipa waandishi wa habari milioni 230/-

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Kanda ya Dar es Salaam, imeiamuru Kampuni ya Quality Group Limited kuwalipa waandishi wa habari 23 iliowaachisha kazi mwaka 2017, jumla ya Sh. 232,324,172.96 (Sh. milioni 232.324).

Tume hiyo inayofanya kazi kama Mahakama ya Mwanzo ya Migogoro ya Kazi, iliiamuru kampuni hiyo kuwalipa waandishi hao kiasi hicho cha pesa, baada ya kuridhika kuwa ilivunja mikataba nao kwa kuwaachisha kazi bila sababu maalumu.

Ilifikia uamuzi huo baada ya wanahabari hao kufungua shauri la mgogoro wa kikazi, wakipinga uamuzi wa kampuni hiyo kuwaachisha kazi kabla ya muda wa mikataba yao wa miaka miwili kuisha.

Wanahabari hao walikuwa wakifanya kazi katika Gazeti la JamboLeo, lililokuwa likimilikiwa na kampuni hiyo, mlalamikiwa akitoa sababu kwamba alikuwa amesikia mambo mazuri kuwahusu wao.

Katika shauri hilo, wanahabari hao, Joseph Lugendo na wenzake 22 walidai kuwa waliajiriwa na mdaiwa huyo kwa nyakati tofauti kwa mikataba ya miaka miwili, lakini Septemba 19, 2017 hata kabla muda wa mikataba yao haujaisha, mdaiwa aliwaachisha kazi.

Hivyo, pamoja na mambo mengine, walikuwa wakiiomba tume hiyo iiamuru kampuni hiyo iwalipe fidia kwa uvunjaji wa mkataba kabla ya muda na malipo ya mishahara ya miezi iliyokuwa imesalia kabla ya mikataba yao kufikia mwisho.

Pia, walikuwa wakidai nyongeza ya mishahara kulingana na makubaliano ya kimkataba, cheti cha huduma, fidia ya madhara ya jumla, malipo ya mishahara hadi tarehe ya uamuzi wa shauri hilo na ujira maalumu (kamisheni).

CMA katika tuzo (uamuzi) yake ya Juni 24 mwaka jana kupitia Msuluhishi Kokusiima L, ilikubaliana na madai na maelezo ya ushahidi wa walalamikaji hao kuwa kilichofanywa na mlalamikiwa ni uvunjaji mkataba kwa kuwa hakuzingatia sheria.

Alisema kuwa hapakuwa na sababu halali ya usitishaji wa mikataba ya walalamikaji kabla ya muda kuisha.

Aliongeza kuwa sababu aliyoitoa mlalamikiwa ni kinyume cha kifungu cha 8(1)(d) cha Kanuni za Ajira na Uhusiano Kazini na Kanuni za Utendaji Bora za Mwaka 2007.

Msuluhishi alifafanua kuwa sababu aliyoitoa kwamba amesikia kitu kizuri kutoka kwa wafanyakazi wenzao ni tata kwa kuwa hakuna namna ambavyo mtu anaweza akaachishwa kazi kwa kusikia habari nzuri kuhusu yeye. Kwa mujibu wa CMA, mlalamikiwa hakuzingatia sheria ambayo inataka kutoa taarifa ya siku zisizopungua 28.

Hata hivyo, Msuluhishi Kokusiima alisema kwa kuwa mikataba ya walalamikaji ilikuwa ni ya muda maalumu, basi kanuni ya kuachishwa kazi kusiko kwa haki haiwezi kutumika na kwamba walalamikaji wana haki ya kulipwa mishahara ya miezi iliyokuwa imebakia tu.

# Mradi wa umeme Julius Nyerere kukamilika Okt. 25

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SHIRIKA la Umeme nchini (TANESCO), limesema ujenzi wa handaki kwa ajili ya kuchepusha maji ya mto katika mradi wa kufua umeme wa bwawa la Mwalimu Julius Nyerere umefikia asilimia 95 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Oktoba 25, mwaka huu.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa usambazaji na huduma kwa wateja, Raymond Seya, alisema hayo wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo kuelekea kipindi cha mvua.

"Ujenzi wa handaki hili ndio ilikuwa changamoto kubwa, lakini sasa tunatarajia ikifika tarehe 25 mwezi huu wa kumi utakuwa umeisha tayari kuchepusha maji ili kutoa fursa sasa ya kujenga tuta kubwa ambalo ndio litazuia maji na kutengeneza bwawa lenyewe," alisema Seya.

Kadhalika, mkandarasi wa mradi amejipanga kuhakikisha mvua zinazondelea kunyesha za masika hazileti athari kwa kuendelea na ujenzi wa ukuta utakaosaidia mto kutoleta madhara katika ujenzi wa bwawa hilo.

Alifafanua kuwa kipindi cha masika ujenzi wa bwawa hautasimama kwasababu tahadhari zote zimeshachukuliwa.

Mkuu wa kazi za ujenzi wa kitengo cha ushauri kihandisi, Mhandisi Rutengano Mwandambo, alisema kazi ya ujenzi inaenda kwa kasi kubwa na kuishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa wakati.

Alisema baada ya serikali kufanya malipo hayo, wakandarasi wanafanya kazi muda wote.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kaze asibebeshwe mzigo mzito Yanga

**BAADA** ya mchakato wa mara ya kwanza kushindwa kufanikiwa, hatimaye klabu ya Yanga imefanikiwa kumpata kocha iliyokuwa inamuwania kwa muda mrefu, Mrundi Cedric Kaze.

Kutua kwa Kaze ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili wa kukinoa kikosi hicho, kunatokana na Yanga kuachana na aliyekuwa Kocha Mkuu, Mserbia Zlatko Krmpotic, ambaye aliiongoza klabu hiyo katika raundi tano za Ligi Kuu Bara.

Ingawa sababu hasa ya kutimuliwa kwa Krmpotic haikuwekwa bayana, lakini vyanzo vya uhakika ndani ya klabu hiyo vilieleza ni kutokana na kushindwa kuiunganisha timu hiyo na kucheza soka la kuvutia ama kwa lugha ya kisoka mitaani wakiliita 'soka la biriani'. Kitakwimu, hatuwezi kumbeza Krmpotic hata kidogo, kwani tunatambua mchango mkubwa alioutoa katika klabu hiyo kwa kuiwezesha kushinda mechi nne na sare moja kwenye michezo mitano aliyoiongoza hadi anaondoka, huku akiwa hana rekodi ya kupoteza hata mechi moja ikiwa ni pamoja na zile za kirafiki walizocheza.

Ingawa tangu awali, Kaze ndiye aliyekuwa chaguo la kwanza kwa Yanga kabla ya kupatwa na matatizo ya kifamilia na kushindwa kujiunga na timu hiyo, lakini Krmpotic hakuwa kocha mbaya, isipokuwa mihemko ya baadhi ya wanachama na mashabiki ndiyo iliyowafanya hata viongozi wa klabu hiyo kumrudia Mrundi huyo baada ya kutatua matatizo yaliyokuwa yakimkabili.

Ikumbukwe, Krmpotic alijiunga na timu hiyo bila kuwa na muda wa kuiandaa kuelekea msimu mpya, hivyo muunganiko wa timu na kuwajua wachezaji, alilazimika kuupata kadri ligi ilivyokuwa inaendelea, lakini pia Yanga ikiwa imesajili wachezaji wengi wapya ambao bado hawajazoeana vizuri.

Lakini pia malengo makubwa ya Yanga, ambayo yamekuwa yakielezwa na uongozi wa klabu hiyo, ni kuhakikisha msimu huu klabu inatwaa ubingwa, ambao kwa misimu mitatu mfululizo, wamekuwa wakishuhudia ukitwaliwa na watani wao wa jadi, Simba. Tunafahamu katika mazingira kama hayo, kikubwa kwa kocha yeyote, kwanza ni lazima ahakikishe timu inashinda ili kujiweka katika nafasi nzuri ya mbio za ubingwa, lakini wakati huo huo akiwa anajaribu kuingiza falsafa zake ili kuiwezesha kucheza soka la kuvutia ambalo linafuata baada ya kuvuna pointi.

Hicho ndicho alichokifanya Krmpotic na kufanikiwa kwa zaidi ya asilimia 90, kutokana na ushindi wa mechi nne na sare moja aliyopata katika mechi tano alizoiongoza klabu hiyo, hivyo kwa suala la muunganiko na soka hilo la 'biriani', ni hatua ambayo ilikuwa inafuata kwani inahitaji muda mwingi kwa wachezaji kuzoeana na kufanya mazoezi kwa pamoja.


Hivyo, pamoja na ujio wa Kaze ambaye amefanya kazi kwa muda mrefu katika akademi za kulea vipaji kwa klabu kubwa Ulaya ikiwamo Barcelona ya Hispania, tunaamini kwa soka la kuvutia ama 'biriani' ni kitu tunachokitarajia kukiona Yanga kwa siku zijazo, lakini pia si suala la haraka kama ambavyo mashabiki wa timu hiyo wanatarajia kwa sasa.

Tutambue soka si kama chumvi ambayo unaitia kwenye mboga na kupata majibu hapo hapo kwamba imekolea ama la, hili ni suala linalotakiwa kwanza mchezaji apate muda wa kuelewa aina ya uchezaji wa wenzake, lakini pia falsafa za kocha ama uchezaji wa timu husika.

Kwa mashabiki wa Yanga, kwa sasa kutamani ubingwa lakini pia wakitaka kuona timu inavuna pointi katika kila mchezo na kucheza soka la kuvutia, jambo ambalo litakuwa mzigo mzito kwa Kaze ambaye ndiyo kwanza ametua huku ligi ikiendelea, lakini pia timu ikiwa na wachezaji wengi wapya ambao hawajazoeana na hata hicho kikosi cha kwanza chenyewe hakijaeleweka.

Tunatambua mashabiki wa Yanga presha yao kwa kocha inatokana na ubora wa Simba, hivyo kutamani kuona timu yao ikicheza soka la 'biriani' kama ilivyo kwa watani zao hao, lakini hawana budi kutambua 'Wekundu wa Msimbazi' hao, wachezaji wao wamekaa pamoja kwa muda mrefu na usajili wanaofanya kila msimu huongeza wachezaji wasiozidi watano tofauti ilivyo kwao, hivyo Kaze hana budi kupewa muda huku presha zikipunguzwa katika kazi yake kwa msimu huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Yanga msitake haraka timu icheze midundo ya wengine

**HATIMAYE** klabu ya Yanga imempata kocha iliyokuwa inamuwania kwa muda mrefu, Cedric Kaze, raia ya Burundi.

Kaze ndiye awali alikuwa chaguo la Yanga, kabla ya kukumbwa na matatizo ya kifamilia, hivyo nafasi yake ikachukuliwa na raia wa Serbia, Zlatko Krmpotic. Ni kama vile haikuwa riziki kwa Mserbia huyo, kwani hakudumu sana kwenye klabu hiyo na yule yule aliyetakiwa awali akachukua nafasi yake.

Inavyoonekana ni kwamba wanachama na mashabiki wa Yanga tayari wameweka matumaini makubwa kwa kocha huyo ili kuwatoa hapo walipo na kuwapeleka wanapopataka.

Ukiwasilika wanachama na mashabiki wa Yanga ni kama vile tayari wanaona wamepata muarobaini wa kumaliza ukame wa ubingwa, pamoja na ukosefu wa kucheza soka safi tayari umeshapatikana kwa asilimia zote.

Ukweli ni kwamba Kaze ni kocha mzuri na analijua soka la Afrika kwa kuwa na yeye ni Mwafrika na mazingira haya anayafahamu, lakini siku zote soka siyo kama chumvi au sukari ambayo ukiweka kwenye mboga au chai basi itakuwa imekolea mara moja. Mimi nadhani Wanayanga kwanza wanapaswa watulie na wamuache kocha aanze kwa kukisuka kikosi ambacho hadi kukaa sawa kinahitaji muda.

Sitarajii mechi ya kwanza tu au ya pili tayari watu wawe wameshaanza kumhukumu kocha huyo kutokana na matokeo, au aina ya soka ambalo litachezwa.

Hakuna kitu ambacho kinaweza tu kuanza mara moja kikawa. Iwe kujenga nyumba, kupika chakula au kutengeneza kitu chochote kile, kuna njia zinapitiwa hadi kufika kunapotakiwa.

Ukiangalia hata kocha aliyepita wa Yanga, sidhani kama alikuwa na matatizo makubwa sana, ila mihemko ya baadhi ya wanachama na mashabiki ndiyo iliyowafanya hata viongozi wa klabu hiyo kuchukua uamuzi huo.

Huwezi kuamini kuwa kocha ambaye ameiongoza timu kucheza mechi sita, ikishinda tano na sare moja anatimuliwa kwenye klabu kwa sababu ambazo hazieleweki vizuri.

Mabingwa Watetezi, Simba, nao pia wamecheza mechi sita, kushinda tano na sare moja kama Yanga, lakini wala hakuna aliyemnyooshea kidole kocha wao, Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Kasoro ya Simba na Yanga ni moja tu kuwa moja ina mabao 14 na nyingine inayo saba. Hata ukiangalia kwenye ulinzi, Yanga bado inaonekana ina ukuta imara zaidi ikiwa imeruhusu bao moja tu, tofauti na Simba iliyoruhusu mabao mawili.

Wengi wanadai kuwa Zlatko ametimuliwa kwa sababu Yanga haichezi vizuri na hadi leo imekuwa haina muunganiko. Hapa ndipo ninapoona kuwa Yanga inacheza midundo ya Simba. Wanachama na mashabiki wa Simba kwa sasa wamekuwa wakipata furaha wanapoiona timu yao mbali na kupata ushindi mnono, lakini pia kucheza kandanda safi na la kuburudisha.

Maneno na tambo za mashabiki wa Simba zinaonekana kuwaingia mashabiki wa Yanga kiasi kwamba na wao wanatamani na kushinikiza wacheze kama Simba. Hii haiwezekani kwa sasa.

Bado Yanga ina wachezaji wengi wapya ambao hawajazoeana. Ni kama vile wametengeneza timu mpya ambayo inahitaji muda ili wachezaji waweze kuzoeana.

Yanga imesajili wachezaji wengi wazuri msimu huu, lakini pamoja na hayo, wengi wamesajiliwa mwishoni, huku timu ikiwa haijapata kocha. Hili nalo lilikuwa athari kubwa kwa klabu hiyo na hata alipowasili kocha bado alikuwa hajakaa na wachezaji wake kupata yale mazoezi magumu ya mwanzo wa msimu.

Pamoja na hayo kocha huyo alijitahidi kwa kila hali kuhakikisha timu inapata matokeo, licha ya soka lisiloridhisha kama inavyodaiwa. Midundo ya mashabiki wa Simba kuwabeza wapinzani wao na wao kujisifia ndiyo inawatesa Yanga kiasi cha kushindwa kuwa na subira. Haiwezekani Yanga hii yenye wachezaji wengi wapya icheze kama Simba ambayo ina misimu mitatu ikiwa na wachezaji wengi wale wale.

Ukiingalia Simba hii, bado ina wachezaji wengi wa misimu mitatu au zaidi iliyopita, kama kina Jonas Mkude, Hamisi Ndemla, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Mzamiru Yassin, halafu wakaja kina Paschal Wawa, Aishi Manula, Erasto Nyoni, John Bocco, baadaye kina Meddie Kagere, Claotus Chama na wengineo.

Pamoja na kusajili wachezaji wengi wazuri wapya, lakini Simba imekuwa ikitumia wachezaji walewale waliozoeana na wale waliosajiliwa wakiingizwa mmoja mmoja ili kuzoea mazingira, kuzoeana na wenzao na aina ya uchezaji wa timu.

Hii ndiyo inawasaidia sana kiasi cha mashabiki wao kufurahia aina ya soka wanalocheza kwa sababu linawajumuisha si tu wachezaji wenye uwezo mkubwa wa soka, lakini pia waliokaa pamoja kwa muda mrefu.

Kwa hali hii, Yanga isitarajie kufumba na kufumbua kuweza kufanya kama wenzao, bali kinachotakiwa kwanza ni kutafuta matokeo na kumpa muda kocha Kaze ili kukijenga kikosi.

Kama wanachama na mashabiki wa timu hiyo wakifuata midundo ya Simba kutaka timu yao ianze kucheza soka la 'biriani' kama wanavyoliita wenyewe kwa muda mfupi tu, basi hata kocha huyu naye muda si mrefu wanaweza kuanza kumtoa kasoro.

Kikubwa kwa sasa ni kumpa muda na mashabiki kukubali kuvuta subra, kwani hakuna soka zuri linalotengenezwa kwa muda mfupi.

# Askofu ataka wananchi kutumia fursa bila kujali dini

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Tanganyika Magharibi, Sadock Makaya, amesema amesikitishwa na baadhi ya wananchi kukataa fursa za maendeleo zinazotolewa na taasisi za kidini ikiwamo ufadhili.

Askofu Makaya aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa mradi wa kisima cha maji kilichojengwa kwa Sh. milioni 42 na Kanisa la Anglikana Mwandiga kwa kushirikiana na huduma ya mtoto chini ya ufadhili wa Shirika la Compasion International Tanzania.

Alisema baadhi ya wazazi, wanawatoa watoto waliopata ufadhili wa kusomeshwa kupitia kituo hicho kwa kisingizio cha tofauti za dini na kuwanyima haki yao ya msingi wakati familia zao zikiwa hazina uwezo wa kuwatimizia ndoto zao za elimu.

Aliiomba jamii kubadilika na kutambua kuwa suala la maendeleo halina dini hivyo mtu yeyote kutoka dini yoyote anapoona fursa muhimu ya kupatiwa elimu aichangamkie.

"Huzuni yangu kubwa na masikitiko ni watu kuwaondoa ati kwa kufikiri kwenye huduma ya mtoto tunawabadilisha dini, hapana sisi tunamwelimisha mtoto kutoka chekechea hadi atakaposhindwa mwenyewe," alisema Askofu Makaya.

Naye Mkurugenzi wa kituo cha huduma ya mtoto, Lilian Magesa, alisema miongoni mwa huduma wanazozitoa kwa jamii ni ufundi cherehani kwa wanawake, mafunzo ya kompyuta na ufadhili wa gharama za masomo kwa watoto.

Alisema kwa miaka mitatu tangu huduma hiyo ianze, watoto 10 wametolewa kwenye mpango wa ufadhili na wazazi wao kwa sababu za tofauti za dini.

"Lengo letu si kuwabadilisha dini watoto bali kuwasaidia ili watimize ndoto zao hasa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu," alisema.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo ya ufundi cherehani, Christana Hosea, alisema uwepo wa taasisi mbalimbali zinazochochea maendeleo kwenye jamii ni ukombozi kwa makundi ya watu wasiomudu gharama za maisha kwa kuwa wanajengewa ujasiri wa kujitegemea.

Alisema, mawazo potofu ya utengano yanasababisha jamii kuendelea kuwa tegemezi na kutaka jambo hilo kupingwa.

Miongoni kwa wanufaika wa mradi wa maji, mkazi wa Mwandiga, Sophia Steven, alisema baada ya uwapo wa huduma hiyo wameanza kupata nafuu ya kero ya maji kutokana na eneo hilo kukosa huduma hiyo.

"Kwa kweli tulikuwa tunapata shida sana ya maji, tulikuwa tunayafuata Mung'onya, ukienda ni karibu saa mbili hujarudi nyumbani," alisema.




Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakamwa, akizungumza wakati wa Kongamano la wafanyabiashara wakubwa na wa kati lililofanyika mkoani Mtwara jana. Benki ya NMB ilikutana na zaidi ya wafanyabiashara 900 kutoka mikoa ya Kusini wa lengo la kuboresha uhusiano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# AMCOS zapewa somo ulipaji wakulima korosho

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

VIONGOZI wa vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) wa mikoa ya Kanda ya Kusini ambayo inazalisha korosho, wametakiwa kuhakikisha wanaandika majina sahihi ya wakulima pamoja na akauti namba zao kwa usahihi.

Wameelezwa kuwa kuandikwa kwa usahihi majina na namba za akaunti, kutaondoa usumbufu wa fedha kushindwa kuingizwa kwenye akauti ya mkulima ikiwa pamoja na kutokuwapo kwa malalamiko ya ucheleweshwaji wa malipo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Meneja Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, wakati akizungumza na wafanyabiashara na wateja wa benki hiyo kwenye jukwaa la klabu ya Wafanyabiashara (BUSINESS CLUB) wa mikoa ya Lindi na Mtwara.

Shango alisema katika msimu uliopita wa mwaka 2019/2020 walikutana na changamoto ya fedha kushindwa kuingia kwenye akaunti za wakulima kwa wakati kutokana na majina ya akaunti kutofautiana na majina ya wakulima na baadae kupelekea baadhi ya wakulima kulalamika kucheleweshewa malipo yao.

"Ili kuondokana na changamoto hii, tayari tumetoa elimu kwa viongozi wa AMCOS pale ambapo wanawaandikisha wakulima wahakikishe wanaandika jina sahihi la mkulima pamoja na akaunti namba yake ikiwezekana amuonyeshe kadi yake ili aweze kuandika namba na jina lake kama lilivyopale," alisema.

"Lakini mbali na hiyo tumekubaliana na viongozi wa AMCOS kuleta majina ya malipo yao kabla ili yaweze kufanyiwa uhakiki, ambapo zoezi hilo tumeshalianza, hivyo kwa msimu huu hatutegemei tena kukutana na changamoto ya pesa kushindwa kuingizwa kwenye akaunti ya mkulima tena," alisema Shango.

Hata hivyo Shango alisema kuwa benki imejipanga katika msimu huu wa malipo kuhakikisha huduma zinakwenda kwa haraka hasa malipo ya wakulima kuwafikia kwa wakati ambapo benki hiyo imeongeza watoa huduma katika matawi yake kwa mikoa yote.

Mkuu wa Idara ya hatari na majanga katika mikopo NMB, Oscar Nyirenda, aliwataka wakulima na wateja wa benki hiyo kuanza kutumia huduma ya bima ambayo NMB imeanza kuitoa ili kuweza kujilinda na majanga mbalimbali wanayoweka kukutana nayo katika shughuli zao za kujikwamua kiuchumi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, ambae alikua mgeni rasmi katika kongamano hilo, aliipongeza benki ya NMB kwa kuamua kukutana na wafanyabiashara jambo ambalo linaonesha namna benki hiyo inavyowajali wateja wao.

"Huduma ya bima ni muhimu kwa sisi wafanyabiashara, mfano vyombo vya moto muda wote vipo barabarani, unaweza ukapata ajali, unaweza ukagonga unaweza ukaanguka, kwahiyo ukikata bima ya chombo chako unarejeshewa, kulingana na bima uliyokata," alieleza Mwanahiza Mdee, mfanyabiashara.

# Mwalwage aiomba NEC uchaguzi uwe wa amani

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kyela kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Alinanuswe Mwalwage, ameiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuzingatia kanuni na sheria kwa kutenda haki kwa wagombea wote ili uchaguzi umalizike kwa amani na utulivu.

Akizungumza jana na mamia ya wananchi wa Kata ya Mwanganyanga Kyela mjini kwenye mkutano wa kampeni, alisema hatua iliyofikiwa ya kupiga kura na kutoa matokeo ni ya muhimu ambayo Tume inapaswa kutenda haki ili amani iendelee kutamalaki.

"Tumeanza kupata mashaka wasimamizi wa vituo kuanza kuulizwa kama wana itikadi za vyama, jambo ambalo tunadhani halijakaa sawa, NEC ijikite zaidi kusimamia sheria badala ya kuwa sehemu ya kuvunja sheria," alionya.

Mwalwage alisema, wananchi wa Jimbo la Kyela, wanapenda kutii sheria bila shuruti na kwamba NEC inapaswa kuhakikisha kanuni, taratibu na sheria zinazingatiwa katika uchaguzi ili kuamua mshindi halali. Akizungumzia wajasiriamali, Mwalwage alisema kama wananchi watampa ridhaa atahakikisha wote katika jimbo hilo wanapatiwa elimu sahihi ya uendeshaji wa biashara ambayo itawaletea manufaa zaidi.

Alisema kwa sasa wajasiriamali wengi wanaendesha biashara zao bila kuwa na elimu sahihi jambo ambalo linawakwamisha washindwe kupata maendeleo ya haraka katika biashara zao.

"Nikichaguliwa nitatumia utaalam wangu kuwapa elimu ya ujasiriamali maana wakipata elimu hata ukimpa mkopo ataweza kuendesha vizuri biashara take," alisema.

Vile vile, alisisitisa suala la kuboresha miundombinu ya barabara katika jimbo hilo ili barabara ziweze kupitika katika kipindi chote cha masika na kiangazi.

# TASAF yahamasisha vita dhidi ya umaskini

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(TASAF), Ladislaus Mwamanga, amesema jukumu la kuondoa umaskini nchini ni la kila mtu.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Unguja na Pemba mwishoni mwa wiki, Mwamanga alisema kuna haja ya kila mtu katika nafasi yake kuhakikisha kwamba anashiriki katika kuondoa na kupambana na umaskini huo.

Aliwaomba watendaji wa Halmashauri kuhakikisha kwamba wanajiwekea utaratibu wa kuwatembelea walengwa waliopo katika mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na TASAF.

"Tunahitaji ushirikiano wa kila mtu ili kurahisisha hii kazi ya kuondoa umaskini katika nchi yetu, sisi kama TASAF tunafanya jitihada ya kuhakikisha tunamaliza tatizo hili, lakini endapo tutashirikiana kazi hii itakuwa rahisi zaidi," alisema Mwamanga.

"Na ndiyo maana kwa sasa tunawasisitiza watendaji wa halmashauri kuona kazi hii inawahusu na wao, wahakikishe kwamba wanajiwekea utaratibu mzuri wa kwenda kuwatembelea walengwa mara kwa mara na kuwasadia."

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC), Irene Mark, alisema ipo haja sasa kwa maofisa ugani, afya na biashara, kujiwekea utaratibu wa kuwatembelea walengwa mara kwa mara ili kuwaidia kuwapatia elimu ya kitaalam katika shughuli ndogondogo wanazoanzisha kutokana na ruzuku wanayopewa na TASAF.

"Tumewatembelea walengwa, mengi tumeyaona huko na kujifunza kwa vitendo, ila tunatoa wito kwa watalaam kujenga utaratibu wa kwenda kuwatembelea walengwa na kuwashauri namna ya kutunza mifugo kitaalam na wale wanaolima kuhakikisha wanawafundisha kulima kisasa kwa sababu tunaamini kwamba miradi yao hiyo ndiyo mwarobaini wa kuwaondoa kwenye umaskini," alisema Mark.

"Kwa kweli tumeshuhuda mambo makubwa yanayofanywa na walengwa hawa, wengi wameonyesha kwamba wameelewa maana ya mpango huu wa TASAF na wanaonekana kuwa na kiu kubwa ya kuondokana na umaskini."

"Tumeshuhudia baadhi wamefuga mbuzi hadi 30, wengine wameondokana na kuishi kwenye nyumba za matope, sasa wamejenga nyumba nzuri za bati, na sisi pia kama wanahabari tumejifunza jambo kubwa kutoka kwa kundi hili la walengwa ambalo tunamini kila mmoja anahitaji kulifanya katika maisha yake."

# Mwakyembe asema Dk. Tulia ni hazina

**Na Thobias Mwanakatwe,** MBEYA

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amesema Naibu Spika ambaye ni mgombea ubunge Mbeya mjini kupitia CCM, Dk. Tulia Ackison ni hazina ya taifa na kuwataka wananchi wasifanye kosa Oktoba 28, 2020.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na madereva na wanamichezo wa timu ya mpira wa miguu ya kituo cha mabasi cha Nane Nane na kituo kikuu cha mabasi jijini, hapa.

Vile vile, alisema yeye na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, wamemfundisha Dk.Tulia, wanamfahamu ni makini na kwamba kuna kila sababu ya wananchi wa Mbeya kumchagua.

Alisema Mbeya imeweka historia ya kuibua vipaji vya michezo na kuweka rekodi kwa timu iliyopanda toka daraja la pili mpaka kuchukua ubingwa ambayo ni Tukuyu Stars.

Alisema timu haiwezi kuwa ligi kuu na za daraja la kwanza bila kuwa na timu za madaraja ya chini zinazozalisha wachezaji kuingia madaraja ya juu.

Aliwataka wanamichezo kuhakikisha wanadumisha amani na mshikamano hususani katika kipindi cha uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Alisema vijana lazima watambue kuwa michezo inalipa, kinachotakiwa ni kujituma kwa kuwa apo wachezajj ambao wanalipwa mishahara mikubwa zaidi.

Kwa upande wao wanamichezo walimhakikishia Dk. Mwakyembe kwamba suala la michezo wanalipa msukumo ili kuwa na timu kubwa ya mkoa huo ambayo italeta ushindani kwa timu za Mbeya City na Prison.

Nao madereva walimuomba Dk. Mwakyembe kuwasaidia kulifikisha katika wizara husika suala la mikataba ya ajira ambalo limekuwa tatizo la muda mrefu.

Mwenyekiti wa Chama cha Madereva Mbeya, Tukuyu na Kyela, James Angetile, alisema madereva wananyanyasika kwa kutopewa mikataba ya ajira hali inayowafanya kuishi maisha magumu.

"Mhe waziri tunaomba suala hili limfikie Rais Dk. John Magufuli, serikali ituangalie matajiri wetu wawe wanatupa mikataba ya ajira," alisema.



Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Godrick Ngolly, akiagana na mmoja wa wanafunzi aliyehitimu elimu ya darasa la saba ambaye ni mlemavu wa viungo wa shule ya msingi iliyopo Kata ya Mpunguzi, jijini Dodoma jana (juzi) **PICHA PETER MKWAVILA**

# W'biashara madini wakumbushwa kutunza kumbukumbu

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MAMLAKA ya Mapato (TRA), mkoa maalumu wa kikodi Kahama mkoani Shinyanga, imewataka wafanyabiashara wa soko la madini ya dhahabu kutunza kumbukumbu za mauzo pamoja na ununuzi ya bidhaa zao.

Pia, imefanya mkutano wa pamoja na wafanyabiashara wa soko la dhahabu la Kahama, maofisa wa TRA na mawakala wa mashine za kielekroniki (EFD), mjini Kahama kwa lengo la kutoa elimu hiyo.

Meneja wa TRA, mkoa maalumu wa kikodi wa Kahama, Warioba Kanire, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, kuwa elimu hiyo waliyopewa itawasaidia kijitambua katika biashara yao kwa kutumia mashine hizo.

Alisema, kwa kuzingatia biashara ya madini inavyofanyika katika soko la madini mjini Kahama, aliwasihi wafanyabiashara hao kujitokeza kwa wingi kuendelea kutumia mashine hizo kwa usahihi na kutunza kumbukumbu za biashara zao ili iwe rahisi kwao kujua faida inayotokana na biasahara hiyo.

Akitoa ufafanuzi wa mashine hizo na umuhimu wake kwa mfayabiashara anayestahili kutoa risiti, Meneja huyo wa TRA, alisema kuna wakati mfanyabiashara anatakiwa kutumia kitabu cha kutoa risiti cha mkono na kufanfanua adhabu atakayopewa mfanyabiashara asiyekuwa na mashine EFD.

Kwa wasiotumia kitabu cha risiti, alisema kulingana na kifungu namba 36 na kifungu namba 86 cha Sheria ya usimamizi wa kodi ya mwaka 2015, adhabu yake ni kuanzia faini ya shilingi milioni milioni tatu mpaka milioni 4.5.

Kwa upande wake, Meneja Msaidizi wa Ukaguzi wa TRA Kahama, Irene Hance, alisisitiza umuhimu wa wafanyabiashara wa soko la madini kulipa kodi kwa wakati na kwa hiyari ili kujiepusha na riba ikiwa ni pamoja na adhabu zinazoweza kuepukika kwa kuwa wazalendo na kutekeleza sheria za kodi.

TRA juzi ilitoa elimu kwa wafanyabiashara wa soko la madini ya matumizi sahihi ya mashine za kielekroniki ikiwa ni harakati za mamlaka hiyo kuendelea kutoa elimu kwa baadhi ya wateja wake kuhusu kodi.

Wilaya ya Kahama ni ya pili kwa kuwa soko kubwa la madini nchini, linaloongoza ni la mkoani Geita.

HABARI KITAIFA

# Walalamikia kwenda kukoboa nafaka Burundi

Na Shaban Njia, NGARA

WAKAZI wa Kijiji cha Ngundusi, Kata ya Kabanga wilayani Ngara mkoani Kagera, wamesema wamelazimika kupeleka mahindi na mpunga Burundi kukoboa, kutokana na kukosa huduma hiyo kwa kipindi kirefu, na kusababisha kuchangia uchumi wa nchi hiyo.

Walisema kuwa mashine hizo zinamilikiwa na serikali ya Kijiji cha Ngundusi na zilifungwa mwaka 2015 na tangu mafundi walioagizwa na serikali kufika kijijini kwa ajili ya kufunga mashine hiyo, hazikuwahi kuwashwa wala kufanya kazi.

Waliyabainisha hayo jana wakati wa mkutano wa mgombea ubunge wa jimbo la Ngara kupitia CCM, Ndaisaba George, na kumwambia kuwa endapo atashinda uchaguzi mkuu Oktaba 28, mwaka huu ahakikishe analitafutia ufumbuzi suala hilo.

Amos Felix, mkazi wa kata hiyo, alisema kuwa licha ya jitihada za kulima zao la mahindi, mpunga na kutumia gharama kubwa kuwekeza kwenye kilimo hicho, bado wanalazimika kutumia gharama ya kusafirisha mazao hayo kwenda Burundi kwa ajili ya kukoboa.

"Mashine hii tangu imefungwa mwaka 2015 kijiji hapa haijawahi kufanyakazi hata mara moja, uwapo wa mashine hii ilisababisha wakulima tuongeze nguvu katika uzalishaji wa mazao ya kimkakati, lakini bado tunalazimika kusafirisha mazao nchi ya jirani kukoboa," alisema Felix.

Nae Yuditha Paul alisema kuwa kuna trekta ndogo maarufu kama Power tiler ambalo lilitolewa kwa serikali ya kijiji nalo limeegeshwa kwa miaka mitano bila kufanya kazi wakati matumaini yao ilikuwa kutumia trekta hiyo kulima mashamba makubwa na kuongeza kipato kwenye familia zao.

Hata hivyo Paul alimtaka Mgombea endapo atapata ridha ya kuwaongoza kwa kushirikiana na Halmashauri wahakikishe mashine na trekta vinafanya kazi ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kibiashara na sio kwenda kukoboa Burundi tena.

Kwa upande wake Ndaisaba alisema kuwa, atahakikisha anaitatua changamoto hiyo kwa kushirikiana na Halmashauri ili kuendelea kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo hasa mazao ya kimkakati ikiwemo mpunga na mahindi.



Waziri wa Nishati, Dk Medard Kalemani (mwenye miwani), Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dk. Tito Mwinuka (kushoto) pamoja na wataalamu mbalimbali, wakiwa kwenye eneo ambalo nguzo za zege zimehifadhiwa zitakazotumika kwenye mradi wa ujenzi wa kituo cha kupooza umeme kinachojengwa Dege katika Wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanda ya Ziwa kupata mvua kidogo

Na Richard Makore, MWANZA

MAMLAKA ya Utabiri wa Hali ya Hewa kanda ya Ziwa (TMA), imesema mikoa sita inayounda kanda hiyo inatarajia kupata mvua kidogo chini ya wastani wa asilimia 45 kati ya mwezi Oktoba hadi Desemba, mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja wa TMA, Augustino Nduganda, katika kikao cha wadau wa kilimo kilichofanyia jijini Mwanza.

Nduganda alisema utabiri wa hali ya hewa unaonyesha mikoa yote sita ya Mara, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Kagera, na Geita itakuwa na mvua kidogo za vuli.

Aliwaomba maofisa kilimo kutoa elimu kwa wakulima ili waweze kupanda mazao yanayohimili ukame katika maeneo yao. Kuhusu wafugaji alisema hali itakuwa mbaya kwa upande wa malisho ya mifugo yao kutokana na kuwapo ukame na hivyo kukosa nyasi na maji.

Akifungua kikao hicho cha siku moja kilichowakutanisha wadau wa kilimo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Emanuel Tutuba, aliwataka kucgangamkia fursa za kilimo katika eneo hilo. Alisema Mkoa wa Mwanza unategemea kilimo kwa asilimia kubwa ikifuatiwa na ufugaji, uvuvi na uchimbaji wa madini katika maeneo mbalimbali.

Aliwataka wadau hao kujadili kwa kina changamoto na fursa zilizopo ili kusaidia sekta ya kilimo kusonga mbele.

Wadau hao wanatoka vyama vya ushirika, vyama vya wakulima, taasisi zinazofanya utafiti katika sekta ya kilimo, Mamlaka ya Hali ya Hewa pamoja na maofisa kilimo.

# Wanafunzi watakiwa kujiandaa ushindani katika soko la ajira

Na Mwandishi Wetu

WANAFUNZI wa shule za msingi wameshauriwa kujiandaa vyema kwa ajili ya kukabiliana na ushindani katika soko la ajira.

Ushauri huo ulitolewa Jumamosi na Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Mashariki, Mangire Kibanda, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, kwenye mahafali ya 22 ya darasa la saba katika Shule ya Msingi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere iliyoko Mbezi Beach jijini Dar es Salaam.

Kibanda alisema kuwa wahitimu hao wanapaswa kutambua kuwa hiyo ni safari yao ya kwenda mbele, hivyo wanapaswa kuwa na juhudi katika masomo.

Kwa mujibu wa Kibanda, ili kukabiliana na dunia ya utandawazi, wanafunzi wanapaswa kutumia fursa ya kujifunza mambo ya msingi kwa kutumia vifaa vya kisasa. Aliwahimiza wazazi na walezi kuhakikisha wanawapa malezi bora na yenye maadili pamoja na kuwawekea akiba kwa ajili ya elimu.

Alisema benki hiyo ina akaunti maalum kwa ajili ya elimu kwa watoto pamoja na bima ya elimu pale mzazi au mlezi anapofariki au kushindwa kuingiza kipato.

Awali Mkuu wa shule hiyo, Charles Wandi, alieleza maendeleo ya taaluma, na kusema shule imekuwa ikipata matokeo mazuri ya mitihani ya kitaifa tangu kuanzishwa kwake, huku watoto wote wakichaguliwa kwenda sekondari.

Hata hivyo, alisema wanakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwamo nyumba za walimu, bwalo la chakula na uhaba wa kompyuta za kujifunzia. Alitolea mfano matokeo ya mwaka jana ambapo watoto wote 55 walikwenda sekondari.

Hata hivyo, Kibanda alisema kwa kuwa Benki ya CRDB ina utaratibu wa kurejesha faida kwa jamii, itaangalia namna ya kusaidia kukabiliana na changamoto hizo, baada ya kukutana na bodi kwa ajili ya majadiliano.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa shule hiyo, Jenerali Ulimwengu, alisema kuwa wanahitahidi kutoa elimu bora kwa vijana kuwajengea msingi wa elimu ya sekondari na vyuo vikuu vya ndani na nje.

# Wakulima washauriwa kilimo ikolojia

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WAKULIMA wameshauriwa kuacha kutegemea madawa yenye kemikali katika mashamba yao badala yake kujikita katika kilimo ikolojia ili kulinda afya ya watumiaji wa mazao ya chakula.

Sababu nyingine imetajwa kuwa ni utunzaji rutuba katika udongo wa mazingira kwa ujumla.

Rai hiyo ilitolewa na Prof Amandus Muhairwa(SUA), ambapo alisema kuwa katika kipindi cha hivi karibuni, baadhi ya wakulima wamekuwa wakitegemea madawa katika kuzalisha mazao yao jambo ambalo limekuwa ni hatarishi kwa afya za watu

Alisema umuhimu wa kilimo hifadhi ni mkubwa kwa sababu kinamuwezesha mkulima kuzalisha kwa wingi bila kuharibu mazingira, ikiwamo kutumia baadhi ya mimea au hata kutengeneza mbolea za asili ambazo hazina kemikali

"Kuna njia nyingi za kufanya kilimo hifadhi na zikazalisha mazao mengi bila kuharibu mazingira bala ya kutumia madawa yenye kemikali mkulima anaweza kutumia mbolea ya samadi kwanza sio gharama sana kutengeneza, lakini ipo baadhi ya miti ambayo inasaidia kutengeneza chakula kwa mimea mingine," alisema Prof Muhairwa

Janneth Maro, Mkurugenzi wa shirika la kilimo endelevu SAT, alibainisha athari zinazoweza kujitokeza moja kwa moja kutokana na matumizi ya kemikali katika sekta ya kilimo ni pamoja na ongezeko la magonjwa ya moyo na shinikizo la damu

Aliongeza kuwa athari hizo zinaweza kuepukika kwa wakulima wa mazao ya chakula kuhakikisha wanajikita katika kilimo hai ambacho kitawaepusha watu na magonjwa ambayo yanasababishwa na matumizi ya kemikali.

"wakulima wakijikita katika kilimo ekolojia kwanza watazalisha mazao salama, ambayo yatasaidia kupunguza hatari za walaji kupata magonjwa kama ya moyo kisukari na shinikizo la damu, kwa hiyo kufanya kilimo hai pia kunasaidia hata kuwa na uhakika wa soko" alisema Maro

Mmoja wa wakulima, Msakuzi Idd kutoka Kata ya Mkuyuni Halmashauri ya Morogoro, alishukuru kupata elimu juu ya kilimo hifadhi ambapo kupitia elimu hiyo itawasaidia kutunza ardhi yao na kutumika muda mrefu zaidi.

Alisema elimu waliyoipata itasaida kufanya kilimo hifadhi na kuachana na matumizi ya kemikali ni pamoja na upandaji wa miti ambao ina virutubisho kwa mimea mingine, pamoja na uchanganyaji wa mazao kama pilipili, nyanya na kabichi ambayo yanatajwa kuwa na virutubisho vinavyolinda rutuba ya udongo.

# Serikali kufanyia utafiti vivuko

**Na Richard Makore,** MWANZA

KAMPUNI ya Serikali ya Huduma za Meli (MSCL), inatarajia kutengeneza meli mpya nne na kukarabati nyingine tano kwa gharama ya Sh. Bilioni 135 mwaka huu wa fedha ili ziweze kutoa huduma katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana jijini Mwanza, Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL, Eric Hamissi, alisema wametangaza tenda kwa ajili ya kupata Mkandarasi wa kufanya kazi hiyo.

Alisema katika mpango wao wa miaka mitano kati ya 2019 hadi 2024 ni kuhakikisha wanakuwa na meli 22 ambazo zitakuwa zinatoa huduma katika maziwa na bahari.

Alisema wakati anakabidhiwa kampuni hiyo ambayo ni ya serikali ilikuwa na meli moja na kwamba hivi sasa wamefufua zingine nne, hivyo kufikisha meli tano ambazo zinafanya kazi.

Eric alisema lengo la kampuni hiyo ni kuhakikisha inakuwa na meli nyingi ambazo zitafanya kazi kwa safari za ndani pamoja na nje ya nchi.

Akizungumzia kampuni hiyo, Eric alisema wakati anakabidhiwa kampuni ilikuwa na Sh. 16,000 pekee benki na kwamba wafanyakazi wakati huo walikuwa wanadai mishahara kwa muda mrefu.

Eric alimshukuru, Rais John Magufuli kwa kuwapatia Sh. bilioni tatu. ambazo walizitumia kulipa mishahara ya wafanyakazi.

Kuhusu kusafirisha mizigo nje ya nchi, Eric alisema wana mpango huo kwa kuwa Tanzania inazungukwa na nchi tisa za maziwa makuu ambazo wanaweza kuzisafirishia mizigo.

Aliongeza kuwa kampuni hiyo imejipanga kuhakikisha inakuwa na meli ambazo zitakuwa zinafanya kazi ya kusafirisha abiria ndani ya nchi pamoja na mizigo inayokwenda nje.

Eric alisema kutokana na mipango yao kwenda vizuri, mwakani wanatarajia kutoa gawio la faida kwa serikali ili kusaidia maendeleo katika sekta zingine.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia (kulia), akikabidhi moja ya mashine kwa ajili ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (Njiti), katika Kituo cha Afya Inyonga B, wilayani Mlele, Mkoa wa Katavi kwa Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Salehe Muhando mwishoni mwa wiki. Vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 49 vilikabidhiwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkakati kuyalinda maeneo ya wazi waanza

**Na Munir Shemweta,** TABORA

OFISI ya Ardhi Mkoa wa Tabora inaanza mkakati wa kuyatambua maeneo yote ya wazi katika halmashauri za Mkoa wa Tabora na kugawa ramani za maeneo hayo kwa watendaji wa kata ili kuyalinda maeneo hayo yasiweze kuvamiwa.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki mkoani Tabora na Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa mkoa huo, Jabir Singano, wakati akielezea utendaji kazi wa ofisi yake tangu kuzinduliwa rasmi mapema mwaka huu na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ukiwa ni mkakati wa Serikali kusogeza huduma za sekta ya ardhi karibu na wananchi.

Alisema, katika Mkoa wa Tabora kumekuwa na tabia ya uvamizi wa maeneo ya wazi katika halmashauri za mkoa huo na katika kukabiliana na tatizo hilo, ofisi yake imeanza mkakati wa kuyatembelea maeneo yote ya wazi katika halmashauri za mkoa huo na kuanza na Manispaa ya Tabora wakiwa na watendaji kata ili kuyatambua na kuwaonyesha mipaka sambamba na kuwakabidhi ramani ili kuyalinda.

" Moja ya kitu nilichoelezwa na ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Tabora wakati ofisi yetu inaanza kazi, ni suala la uvamizi maeneo ya wazi hivyo tumeamua kulifanyia kazi kwa kuyatambua maeneo ya wazi na kugawa ramani za maeneo hayo kwa watendaji wa kata ili waweze kuyalinda na tumeanza na Manispaa ya Tabora na baadaye tutaendelea na halmashauri nyingine" alisema Singano.

Aidha, Singano alisema mpango mwingine wa ofisi yake ya Ardhi katika kuboresha sekta ya ardhi mkoani Tabora ni kukagua maeneo yote ya umma na kuanza na yale maeneo ya shule za msingi na sekondari kwa kubainisha mipaka ambapo alisema lengo ni kuhakikisha maeneo yote ya umma hayavamiwi wakati ofisi ya ardhi mkoa ipo.

Kwa upande wake Mtendaji wa Kata ya Mpera Manispaa ya Tabora, Grace Kasegezya, aliishukuru ofisi ya ardhi Mkoa wa Tabora kwa kuanza zoezi la utambuzi maeneo ya wazi na kuwapatia ramani zinazoonesha maeneo ya wazi watendaji katika Kata za Manispaa ya Tabora.

Alisema, kuoneshwa mipaka na kupatiwa ramani za maeneo ya wazi katika kata siyo tu kutawasaidia watendaji wa kata kutambua maeneo ya wazi bali kutawawezesha pia kama kuyafuatilia na kuyalinda dhidi ya uvamizi unaoweza kufanywa.

Katika hatua nyingine Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Tabora imeendesha utoaji elimu na kuhamasisha ulipaji kodi ya pango la ardhi katika mitaa mbalimbali ya Manispaa ya Tabora.

Zoezi hilo limeogozwa na Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Tabora Jabir Singano kwa kushirikiana na Maofisa kutoka ofisi yake ya mkoa, halmashari ya Manispaa ya Tabora na Mtendaji wa Kata ya Mpera, Grace Kasegezya.

Nipashe
Spotiki



WACHEZAJI 10 WALIOHUSIKA MABAO MENGI KARNE YA 21 UK. 12




# KWA NINI USAJILI WA CAVANI UNALETA MAANA MAN UTD

**MANCHESTER,** England

SAA 48 kabla ya kufungwa kwa soko la usajili nchini England, Manchester United walikuwa kwenye wakati mgumu wa kutafuta mshambuliaji.

Na katika siku ya mwisho kabisa ya kufungwa kwa pazia hilo, wakafanikiwa kumsajili Edinson Cavani kwa uhamisho huru.

Kwa kipindi kirefu cha dirisha la usajili, Man United walikuwa wakihusishwa na kutaka kuwasajili, Jadon Sancho, huku pia wakimnyatia Ousmane Dembele ili wamchukue kwa mkopo kutoka Barcelona.

Hata hivyo, Borussia Dortmund wakaweka ngumu kumuuza Sancho, huku wao Barcelona wakitaka timu itakayomsajili moja kwa moja Dembele.

Na mwishowe, Man United wakahamishia majeshi kwa Cavani na wakamsajili Facundo Pellistri mwenye umri wa miaka 18.

Pamoja na kushindwa kufanya usajili, 'Mashetani Wekundu' hao wanaonekana kuramba karata nzuri kwa kumsajili Cavani.

## KUIMARISHA MASHABULIZI

Usajili wa Cavani unaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.

Kwani straika huyo wa zamani wa PSG ni mmoja wa washambuliaji wanaolijua vizuri goli na mmaliziaji hatari zaidi.

Usajili wake unaleta maana, kwani kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer kilikosa mshambuliaji wa maana tangu kuondoka kwa Romelu Lukaku kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Raia huyo wa Ubelgiji pengine hakufiti kwenye staili ya uchezaji ya timu, lakini ni bora zaidi ya mara mbili dhidi ya Anthony Martial.

Odion Ighalo alisajiliwa kwa ajili ya kumsaidia Martial, lakini nyota huyo anayecheza kwa mkopo ameonekana sasa kutokuwa kwenye kiwango kizuri.

## UHAKIKA WA MABAO

Kwa uwapo wa Cavani, Mashetani Wekundu hao sasa watakuwa na uhakika wa kupata mabao hasa kutokana na ukweli kwa kile alichokionyesha kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Ligue 1 na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ukiacha msimu uliopita ambao alikumbwa na majeraha ya mara kwa mara, raia huyo wa Uruguay alifunga mabao 15 au zaidi kwa kila msimu kwa misimu 10 iliyopita.

Msimu ambao alifunga chini ya mabao 15 kwenye ligi ni ule wa 2009-10 wakati alipokuwa anaichezea Palermo. Hata hivyo, alifunga mabao 13 kwa kikosi hicho.

Anaweza kuwa na umri wa miaka 33, lakini usajili wake ni muhimu zaidi kama ilivyokuwa kwa Zlatan Ibrahimovic miaka minne iliyopita.

Raia huyo wa Sweden aliwasili pale Old Trafford akiwa na umri wa miaka 35, lakini alikuwa mchezaji muhimu wakati wakishinda taji la Carabao na lile la Ligi ya Europa mwaka 2017.

Cavani anaweza kuwa na mchango kama huo, hasa kutokana na klabu hiyo kutokuwa na mshambuliaji wa maana kwenye timu.

Ni mshambuliaji wa daraja la juu na atatoa presha kubwa kwa Martial msimu huu na kuisaidia timu.

Usajili wa Cavani si kamari, kwani anastahili kutokana na rekodi yake ya huko nyuma katika ufungaji wa mabao.

Amesaini mkataba wa mwaka mmoja wenye kipengele cha kuongeza miezi mingine 12.

Sasa ni suala la muda tu kusubiri kuona namna gani Cavani atakuwa msaada kwa kikosi hicho kwa msimu huu.

## ISIKUPITE

Wakati Pep Guardiola akiongoza Manchester City kushinda bao 1-0 kwenye Ligi Kuu England dhidi ya Arsenal juzi, ushindi huo unamfanya kocha huyo sasa kushinda jumla ya mechi 500 kwenye mashindano yote akiwa kama kocha (idadi hiyo ikijumuisha pia alizoshinda kipindi akiinoa Barcelona B). Kati ya hizo alizoshinda akiinoa Manchester City ni 172.



## Extra Time

# WACHEZAJI 10 WALIOHUSIKA MABAO MENGI KARNE YA 21


LIONEL MESSI

**LONDON,** England

KARNE ya 21 imeibua wafungaji mabao mahiri zaidi ambao wamefunga kwenye mashindano makubwa kwa klabu zao na timu za taifa na kushinda mataji mengi.

**Hata kama hawakufunga, wachezaji hao wataonyesha mchago mkubwa kwa kutoa nafasi kwa wachezaji wenzao kufunga huku wao wakisaidia.**

Makala haya yanawachambua wachezaji 10 ambao wamehusika kwenye mabao mengi zaidi (kufunga na kutoa pasi za mwisho), je, unawajua? Kama sivyo, wajue sasa...

### #10. KARIM BENZEMA (523) – MABAO 343 NA PASI ZA MWISHO 180

Mshambuliaji wa Ufaransa, Karim Benzema, amekuwa pale Real Madrid tangu alipotua klabuni hapo kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2009.

Baada ya kuanza kucheza soka katika Klabu yake ya Olympique Lyon mwaka 2005, alianza kutoa mchango wa mabao kwa mara ya kwanza kwa klabu hiyo ya Ufaransa, wakati aliposaidia Lyon kuibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Metz.

Benzema aliibuka mfungaji bora akiwa na mabao 20 msimu wa 2007-08 wakati Lyon iliposhinda taji lake la saba la Ligi Kuu ya Ufaransa. Haraka Real Madrid wakamuita mwishoni mwa msimu uliofuata, na hakuangalia tena nyuma.

Akiwa na mchango wa mabao 92 (66 ya kufunga na 26 pasi za mwisho) kwa kipindi cha misimu minne aliyocheza pale Ufaransa, Benzema anaendelea na kiwango chake cha kuvutia kwenye dimba la Bernabeu.

### #9. SAMUEL ETO'O (524) – MABAO 408 NA PASI ZA MWISHO 116

Samuel Eto'o pengine ndiye mchezaji bora zaidi wa wakati wote wa Afrika. Wakati wa kipindi chake cha uchezaji, raia huyo wa Cameroon alikuwa na mchango mkubwa na alitengeneza jina lake pale Barcelona.

Real Madrid walimkataa, lakini alipokwenda upande wa pili, Barcelona, mambo yalibadilika kabisa na kuonyesha kiwango chake.

Eto'o ni mmoja wa wachezaji aliyeshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili mfululizo akiwa na timu mbili tofauti. Pia ni mchezaji pekee kushinda Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia mara mbili mfululizo akiwa na klabu mbili tofauti Barcelona msimu wa 2008-09 na Inter Milan msimu uliofuata.

Ameshinda mataji mawili ya mataifa ya Afrika, ameshinda mara nne tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Afrika na ni mfungaji wa wakati wote wa Cameroon akiwa na mabao 56.

### #8. WAYNE ROONEY (545) – MABAO 366 NA PASI ZA MWISHO 189

Wayne Rooney, ambaye alijenga jina lake na klabu yake ya utotoni ya Everton, alianza kufumania nyavu tangu akiwa mchezaji kinda.

Mshambuliaji huyo alijiunga na Manchester United kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2004 na tangu hapo hakuangalia tena nyuma ambapo alicheza kwa misimu 13 kwenye Ligi Kuu ya England.

Rooney, ambaye ni mmoja wa wachezaji walioweka historia ya kufunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na umri mdogo, ni mfungaji bora wa Manchester United (mabao 253) na timu ya Taifa ya England (mabao 53).

Rooney, ambaye kwa sasa anacheza kule katika Klabu ya Derby County katika daraja la kwanza, ni mchezaji wa pili mwenye umri mdogo zaidi kutoa pasi ya mwisho kwenye historia ya Ligi Kuu ya England.

### #7. SERGIO AGUERO (549) – MABAO 414 NA PASI ZA MWISHO 135

Sergio Aguero, ambaye alianza kuichezea timu ya nyumbani kwao Argentina ya Independiente mwaka 2003, alikaa misimu mitano na Atletico Madrid kabla ya kutua pale Manchester City kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2011.

Aguero ni mchezaji wanne mwenye mabao mengi zaidi (180) kwa wageni katika Ligi Kuu ya England.

Aguero, ambaye pia amefunga 'hat-trick' 12 kwenye Ligi Kuu ya England, ameifungia timu ya Taifa ya Argentina mara 42, akiwa nafasi ya tatu nyuma ya Gabriel Batistuta (43) na Lionel Messi (70).

### #6. THIERRY HENRY (559) – MABAO 369 NA PASI ZA MWISHO 190

Baada ya kuanza kucheza soka la kulipwa kule Monaco, Thierry Henry alijiunga na miamba wa soka la Italia, Juventus kabla ya kwenda Arsenal mwaka 1999 na kuweka historia yake.

Mfaransa huyo ambaye alikuwa akicheza kama winga akiwa Monaco na Juventus, alibadilishwa na kocha wa Arsenal, Arsene Wenger na kuwa mshambuliaji wa kati.

Wakati wa misimu nane akiwa na Arsenal, Henry akawa mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo akiwa na mabao 253, huku kwenye timu ya Taifa ya Ufaransa akiifungia mabao 51.

Ni mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 1998 pamoja na lile la Mataifa ya Ulaya alilioshinda mwaka 2000.

Alihamia Barcelona kabla hajatimiza umri wa miaka 30 mwaka 2007 na alikuwapo kwenye kikosi hicho cha Catalunya kilichoshinda mataji matatu msimu uliofuata. Baadaye akaenda kucheza Ligi Kuu ya Marekani katika klabu ya New York Red Bulls kwa misimu mitano kabla ya kustaafu.

### #5. ROBERT LEWANDOWSKI (621) – MABAO 477 NA PASI ZA MWISHO 144

Robert Lewandowski bila shaka yoyote pengine ndiye straika bora zaidi kwa sasa. Raia huyo wa Poland mwenye umri wa miaka 32, ndiye mfungaji wa wakati wote kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, kwa wachezaji wageni.

Nyota huyo wa Bayern ana uwezo mkubwa wa kufunga na nguvu ya kumiliki mpira na ameshinda mataji mengi kwa kipindi chake cha uchezaji katika ngazi ya klabu.

### #4. LUIS SUAREZ (730) – MABAO 463 NA PASI ZA MWISHO 267

Luis Suarez ni straika mwenye historia yake kwa uwezo wa kufunga na kutoa pasi za mwisho kwa wachezaji wenzake.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, ambaye alianza kutamba kule kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivise, akiwa na Ajax, alijiimarisha yeye mwenyewe katika Klabu ya Liverpool akifunga mabao 31msimu wa 2013-14.

Baadaye Suarez akahamia Barcelona ambako walitengeneza upatina mzuri wa safu ya ushambuliaji kati yake na Lionel Messi na Neymar.

Katika misimu sita na miamba hao wa Catalunya, Suarez alifunga mabao 200 katika mashindano yote.

Suarez, ni mmoja wa wachezaji watatu tu katika historia ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kufunga mabao 40 kwa msimu mmoja, kwa sasa amejiunga na Atletico Madrid.

### #3. ZLATAN IBRAHIMOVICH (732) – MABAO 501 NA PASI ZA MWISHO 201

Zlatan Ibrahimovich, mmoja wa wachezaji wanne tu kuweza kutoa pasi za mwisho zaidi ya 200 kwa klabu na nchi yake, na bado yupo imara katika umri wake wa miaka 39.

Katika umri huo washambuliaji wengi wanakuwa wamestaafu, lakini raia huyo wa Sweden kwa sasa yupo katika msimu wake wa pili na AC Milan.

Ibrahimovich amefunga mabao ya Ligi Kuu katika nchi saba tofauti na ameshinda mataji 11 katika nchi nne tofauti, na ya karibu zaidi ni wakati alipotwaa taji la Ligi Kuu akiwa na Paris St. Germain msimu wa 2015-16. Ingawa pia alishinda taji la Ligi ya Europa akiwa na Manchester United msimu wa 2016-17.

Msimu uliopita, aliweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 50 kwa klabu mbili za mji wa Milan - AC Milan (54) nA Inter Milan (57).

### #2. CRISTIANO RONALDO (988) – MABAO 742 NA PASI ZA MWISHO 246

Cristiano Ronaldo, pengine ni mmoja wa wachezaji bora zaidi kuwahi kutokea kwenye historia ya mchezo huo. Kwani amejiwekea rekodi nyingi sana kwenye klabu na timu ya taifa.

Baada ya kuanza kucheza soka lake la kulipwa katika Klabu ya Sporting Lisbon ya nchini kwake Ureno, Ronaldo akairithi jezi namba 7 pale Manchester United na kamwe hajaangalia tena nyuma.

Ni mfungaji wa wakati wote wa Real Madrid na katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa mmoja wa wachezaji walioshinda mataji ya Ligi Kuu katika ligi tatu tofauti kati ya tano kubwa za Ulaya.

Katika umri wa miaka 35 kwa sasa anacheza kule Juventus na ndiye mchezaji pekee wa Ulaya kuifungia timu yake ya taifa mabao 100.

### #1. LIONEL MESSI (1031) – MABAO 705 NA PASI ZA MWISHO 326

Pamoja na Cristiano Ronaldo, Lionel Messi ni mchezaji pekee kufunga zaidi ya mabao 700 kwa klabu na nchi yake. Aidha, Messi ndiye mchezaji pekee aliyehusika katika mabao 1000 katika karne hii ya 21.

Messi ni mfungaji bora wa wakati wote kwenye LaLiga. Nahodha huyo wa Barcelona na Argentina amefunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na klabu moja (115 kwa Barcelona) na ameshinda mataji mengi zaidi ya LaLiga (10) na mshindi mara sita wa Ballon d'Or.

## Nukuu

"KILA wakati una historia yake, kila kizazi kina rekodi zake, alikuwa Ronaldo, kulikuwa na Rivaldo, Romario, Bebeto, kila mmoja kwa wakati wake, si haki kuwalinganisha hawa, kwani kila mmoja na wakati wake na rekodi yake kwenye kikosi cha Brazil. Ninachoweza kusema sasa ni kwamba, Neymar ameweka rekodi yake katika wakati wake. Kwa sasa yeye ndiye mchezaji muhimu kwa Brazil," **Kocha wa Brazil, Tite akimpongeza Neymar kufunga mabao 64 timu ya taifa mawili zaidi ya Ronaldo, sasa akimtafuta Pele mwenye mabao 77.**




"SIJALI kuhusu hilo, kama [Lionel Messi] atakuja litakuwa ni jambo jema na kama hatokuja ni jambo zuri pia, kwa sababu tuna wachezaji wazuri ambao najisikia furaha kucheza nao," **Kiungo wa Manchester City, Kevin De Bruyne, akinukuliwa na Sky Sport wakati akizungumzia uwezekano wa nyota huyo wa Barcelona kutua Etihad.**



"NIMEANZA kwa kiwango cha chini kwa sababu ligi hii ni tofauti kabisa na ile niliyotoka, simaanishi kwamba Bundesliga ni ligi mbaya ama rahisi sana, lakini nimeona tofauti hapa, unapokutana na timu yoyote huwezi kusema ina wachezaji wa kawaida ama wenye viwango vya chini. Ligi ya England ni tofauti kabisa na Bundesliga ambayo aina ya uchezaji wa timu zao ni wa taratibu ukilianganisha na England ambazo zinahitaji mchezaji awe na nguvu na kasi sana," **Kiungo wa Chelsea, Kai Havertz akinukuliwa na gazeti la Bild.**





Kinara wa mabao Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube (kushoto), akishangilia moja kati mabao yake akiwa na straika mwenzake wa klabu hiyo, Obrey Chirwa. **PICHA: MTANDAO**

# RAUNDI YA SITA LIGI BARA KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

TAYARI Ligi Kuu Tanzania Bara imeingia kwenye raundi ya sita, huku timu zingine zikiwa hazijamaliza viporo vyake na zingine leo zikitarajiwa kucheza mechi za raundi ya saba.

Timu za Simba, Yanga, Prisons na Polisi Tanzania, mpaka sasa zimecheza mechi tano tu kila moja, lakini leo raundi ya saba inatarajiwa kuendelea kwa mechi nne, JKT Tanzania ikiikaribisha Prisons kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma, Coastal Union ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Mwakwani Tanga ikialika Biashara United kutoka Mara, Mtibwa Sugar itakuwa nyumbani kuisubiri Namungo FC na Polisi Tanzania itakuwa kwao ikicheza dhidi ya Gwambina.

**Wakati Ligi Kuu ikiingia kwenye raundi ya saba leo kwa baadhi ya timu, tayari kuna rekodi na takwimu mbalimbali za kuvutia, kushangaza na kufurahisha zimejitokeza hadi kufika raundi ya sita zikiwekwa na timu mbalimbali pamoja na wachezaji.**

Makala haya yanakuletea rekodi na takwimu hizo kwa mtindo wa namba, twende sasa...

**84-** Ni idadi ya mabao yote yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

**58-** Hii ni idadi ya wachezaji waliofunga mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa ambayo hadi leo yamefikia 84.

**52-** Ni idadi ya mechi zote za ligi zilizochezwa hadi kufikia raundi ya sita ya Ligi Kuu.

**44-** Hii ndiyo idadi ya wachezaji waliofunga bao moja kila mmoja kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**42-** Inasimama kama idadi ya mechi zote za ushindi zilizofungwa kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**27-** Namba hii ni idadi ya mechi ambazo timu zimeshinda zikiwa kwenye viwanja vyao vya nyumbani.

**18-** Vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC wana idadi hizi za pointi baada ya mechi sita.

**17-** Ni idadi ya wachezaji wa kigeni waliofunga mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

**15-** Ni idadi ya mechi za Ligi Kuu ambazo timu zimeshinda zikicheza ugenini mpaka sasa.

**13-** Hizi ni idadi ya pointi za Simba na Yanga ambazo zimekusanya kila moja, zikiwa zimecheza mechi sita, zikishinda michezo mitano na sare moja kila moja.

**12-** Ni pointi za Azam FC na Biashara United ya Mara zilizozipata zikicheza kwenye viwanja vyao vya nyumbani na kuwa ndizo timu pekee zenye matumizi mazuri ya viwanja vya nyumbani mpaka sasa.

Timu hizo zimecheza mechi nne nyumbani na kushinda zote.

**10-** Namba hii ni idadi ya mechi za sare kwenye Ligi Kuu zilizopatikana hadi leo hii.

**7-** Hizi ni idadi ya mechi ambazo Mabingwa Watetezi, Simba wameshinda wakicheza ugenini na kuwa timu inayoongoza kwa kukusanya pointi nyingi ikicheza nje ya uwanja wake wa nyumbani mpaka sasa. Imechea mechi tatu ugenini, ikishinda mbili na sare moja.

**6-** Ni mabao ambayo ameyafunga kinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube raia wa Zimbabwe, lakini pia ni idadi ya mechi ambazo klabu yake hiyo imeshinda mpaka sasa.

**4-** Ni namba inayoihusu Ihefu FC ambayo imepoteza mechi nne mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Baada ya kufungwa na Simba mabao 2-1 na kushinda bao 1-0 dhidi Ruvu Shooting, timu hiyo iliiona joto la jiwe ilipoanza kupoteza mfululizo dhidi ya Mtibwa Sugar bao 1-0, mabao 2-0 dhidi ya Mwadui, mabao 2-0 dhidi ya Gwambina na bao 1-0 dhidi ya Biashara United.

**2-** Ni penalti mbili zimepatika kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Ya kwanza ilipatikana kwenye mechi kati ya KMC na Coastal Union. Katika mechi hiyo, Coastal ilipata penalti, lakini kipa Juma Kaseja aliokoa baada ya kupigwa na Yusuph Soka, huku ya pili ikitoka kwenye mechi kati ya Gwambina dhidi ya Mtibwa Sugar.

Kwenye mechi hiyo, penalti hiyo ilizaa bao lililofungwa na Yusuph Lwenge, Gwambina ikishinda kwa mabao 2-0.

**1-** Hii inasimama kama bao pekee ambalo imeruhusu Yanga mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Timu hiyo ndiyo imeruhusu bao moja tu, ambalo lilifungwa kwenye mechi ya ufunguzi kati ya timu hiyo dhidi ya Prisons, likiwekwa wavuni na Lambart Sabianka, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1.

**0-** Sifuri hii inasimama kwa Mbeya City kuwa ndiyo timu pekee kati ya 18 zinazoshiriki Ligi Kuu ambayo haijafunga bao lolote mpaka sasa, lakini pia ikiziwakilisha Azam FC, Simba na Yanga ambazo hazijapoteza mchezo hata mmoja.

## JE, WAJUA?



PENALTI waliyozawadiwa Manchester United dhidi ya Newcastle United na Bruno Fernandes na kuikosa wakati wakishinda 4-1 juzi, ni ya 17 kwa mi-amba hiyo ya Old Trafford kuzawadiwa kwenye Ligi Kuu England tangu kuanza kwa msimu uliopita, idadi hiyo ni penalti tano zaidi kuliko ilizozawadiwa klabu nyingine yoyote katika ligi hiyo. Kati ya hizo 17 United imefunga 12 pekee.





# Serikali yaombwa upimaji ardhi vijijini

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JUKWAA la Wakulima Wanawake Tanzania, limeomba serikali kukamilisha upimaji wa ardhi vijijini na kutoa hati miliki za kimila ili wanawake wamiliki ardhi.

Katibu wa Jukwaa hilo, Anastazia Madeje, alitoa ombi hilo wakati akiwasilisha mapendekezo ya wanawake kwenye siku ya mwanamke anayeishi kijijini ambayo hufanyika Oktoba kila mwaka, iliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Actionaid Tanzania.

Madeje alisema asilimia kubwa ya wanawake vijijini wanafanya kazi za kilimo, lakini kwenye ardhi ambayo hawana umiliki.

"Kwa sasa asilimia kubwa ya wanawake wanafanya kazi za kilimo lakini mwisho wa siku wanufaika wakubwa ni wanaume na familia kwa ujumla kwa kuwa mwanamke huyo hana umiliki wa ardhi anayoilima," alisema Madeje.

Alisema kama mwanamke atapata hati miliki ya ardhi ataitumia kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha na kuboresha kilimo chake kuwa cha kisasa na kuzalisha kibiashara.

Madeje alisema wanawake wengi wa vijijini kwa sasa wanazalisha kwa ajili ya chakula na si kibiashara na hivyo kufanya shughuli zake zote za kilimo kwa ajili ya familia na si kwa ajili ya kuzalisha fedha zake binafsi.

Naye, Mkulima Dorah Myinga, alisema ni vyema serikali ikatoa vipaumbele kwa wakulima wanawake waliopo vijijini hasa kwenye masuala ya mbegu na pembejeo kwa kuwa wao ndio wazalishaji wakubwa kwa mazao ya chakula na biashara.

Kwa upande wake, mtaalamu wa masuala ya kijinsia kwenye sekta ya maendeleo, Anna Mushi, alisema asilimia 54 ya nguvukazi kwenye kilimo ni wanawake ambao wengi wao hawana elimu ya kutosha.

Alisema asilimia 57 ya wanawake wanaoishi vijijini ni wale ambao wamemaliza darasa la saba na wanajua kusoma na kuandika na kusababisha wengi wao kutokuwa na elimu kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na jinsi ya kukabiliana nayo.

"Shughuli kubwa ya mwanamke wa kijijini ni kilimo iwe ni kwenye shamba la familia yake au kibarua kwa mtu mwingine na ndiyo maana maisha yao si mazuri kwa kuwa hata huko kwenye vibarua wanalipwa malipo kidogo tofauti na wanawake," alisema Mushi.

Alisema kutokana na hali hiyo, hakuna mwanamke wa kijijini ambaye atakopeshwa na taasisi za kifedha na kwamba suluhisho pekee ni kupatiwa hati miliki ya kimila ili kulima kisasa kwa ajili ya mazao ya kibiashara.



Wanachama wa Chama cha ACT Wazalendo wa Mtaa wa Mahomanyika Kata ya Chahwa, Jiji la Dodoma, wakimnyanyua juu mgombea wao anayewania nafasi ya udiwani Andrea Ngoligo, baada ya kumalizika kwa mkutano wake wa kampeni uliofanyika viwanja vya mtaa jana. **PICHA PETER MKWAVILA**

# H/shauri Bahi kujenga kiwanda kuchakata ngozi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bahi, inatarajia kujenga kiwanda cha kuchakata ngozi chenye thamani ya Sh.Bilioni 3.3, kutokana na kuwapo kwa fursa kubwa ya uwekezaji kwenye eneo hilo.

Mkurugenzi wa Mtendaji Halmashauri hiyo, Dk. Fatuma Mganga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wilayani humo alipokuwa akizungumza na wafugaji. Alisema sekta ya ngozi ni moja ya fursa kubwa ya uwekezaji katika wilaya hiyo kutokana na wingi wa mifugo inayochinjwa kwa mwaka.

Alieleza kuwa wastani wa ng'ombe 1,085 na mbuzi na kondoo 2,253 huchinjwa kwa mwezi, hivyo kuna fursa hiyo kuwekeza kwenye viwanda vidogo na vikubwa vya kusindika na kuchakata ngozi na mazao yake.

"Halmashauri imeshaandika andiko la mradi wa kiwanda cha kuchakata ngozi lenye thamani ya Sh.Bilioni 3.3 tayari andiko hili lipo Wizara ya Fedha kwa ajili ya mapitio kabla ya fedha kutolewa," alisema.

Aidha, Dk. Mganga alisema ufugaji ni moja ya shughuli kuu mbili za kiuchumi kwa wananchi wa wilaya hiyo, na kwamba mifugo huchangia zaidi ya asilimia 55 ya mapato ya ndani ya Halmashauri hiyo.

"Wilaya ina hazina kubwa ya mifugo ambapo asilimia 96 ya mifugo inayofungwa ni ya asili na asilimia nne ni ng'ombe walioboreshwa," alisema.

Hata hivyo, alisema katika jitihada za kuongeza idadi ya mifugo iliyoboreshwa Halmashauri kwa kushirikiana na wafugaji imeanza kuboresha kosafu za mifugo kwa kutumia njia ya uhamilishaji ambapo hadi sasa wafugaji nane wamekubali na wanatekeleza mpango huo.

"Jumla ya ng'ombe 67 zimehamilishwa kwa mwezi Julai mwaka huu, lengo likiwa ni kumfanya mfugaji afuge ng'ombe ambao wanafikia uzito wa soko mapema na wenye kutoa maziwa kati ya lita 8 hadi 10 kwa siku," alisema.

# Prof. ashauri jamii kuwekea akiba watoto

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKUU wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, Prof. Hozen Mayaya, ameitaka jamii kujenga utamaduni wa kuwawekea akiba ya fedha na mali watoto wao kwa kipindi chote wanachokuwa masomoni ili kufikia ndoto zao.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano wa Chuo hicho, Godrick Ngoli kwa niaba ya Prof. Mayaya kwa wazazi, walezi wa Kata ya Mpunguzi jijini Dodoma kwenye mahafali ya darasa la saba.

Katika hotuba yake, Prof. Mayaya alisema kuna baadhi ya wazazi, walezi wenye watoto wanaosoma shule za sekondari na vyuo vikuu wanashindwa kuwaendeleza kielimu kutokana na tatizo la ukosefu wa fedha.

Alieleza kitendo cha kuwawekea akiba kitasaidia kuwalipia kidato cha tano na sita na kwa wale watakaojiunga na vyuo vikuu katika mahitaji yao wanayohitaji kulipa.

"Hivyo suala la kujijengea tabia ya kujiwekea akiba liwe la utamaduni kwa kila mzazi na mlezi, hii itaweza kuwasaidia pindi mwanafunzi kusoma na kufikia ndoto yake ili kulitumikia Taifa lake kwa malengo ya kuleta maendeleo yake mwenyewe, wazazi na hata kwa Taifa pia," alisema.

Aidha, aliwasa wahitimu kutojihusisha na makundi maovu ambayo yatakatisha ndoto walizokuwanazo za kujiendeleza zaidi kielimu.

"Wazazi kuhakikisha mnawaendeleza kielimu zaidi hawa watoto badala ya kufikiria kuwatafutia kazi za majumbani, kuchunga na wengi kuwaozesha," alisema.

Mmoja wa wahitimu, Jerimia Malugu, alisema baadhi ya wazazi bado wana mtazamo hasi kwa kuwachukulia watoto wanaomaliza elimu yao kama mtaji kwa kuwatafutia vibarua.

Malugu aliomba serikali kuanzia ngazi za mitaa hadi za juu, kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaoshiriki kukwamisha ndoto za wanafunzi.





# Tulia aahidi maendeleo Jiji la Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA Ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Tukia Ackson, amesema endapo atachaguliwa, atahakikisha anashirikiana na Serikali pamoja na wananchi wa Jiji la Mbeya kuleta maendeleo.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na wananchi wa Kata ya Kalobe kwenye mkutano wa hadhara wa kuomba kura ambapo alisema kabla hajawa mbunge wa Jimbo hilo alifanya maendeleo kwenye maeneo mbalimbali na hivyo akichaguliwa itakuwa zaidi.

Alisema katika sekta ya elimu pekee alitumia zaidi ya Sh. milioni 205 ikiwemo ukarabati wa miundombinu, ununuzi wa vifaa mbalimbali pamoja na tuzo za walimu ambazo huwa zinafanyika kila mwaka mkoani humo.

Alisema kuna baadhi ya watu wanapita kwa wananchi wakiwashawishi kuwa wasimchaguwe kwa sababu yeye ni mwanamke na hivyo akawataka wananchi kuwapuuza watu hao na kuendelea kumwamini na kumchagua.

"Kipindi hiki ni kipindi cha hesabu, ambaye hakufanya kazi wananchi sukuma nje na nawahakikishia kwamba mimi nitakuwa mbunge wa kujiongeza ili tupate maendeleo na kulibadilisha Jiji letu, sitategemea fedha za mfuko wa jimbo," alisema Dk. Tulia.

Alisema fedha za mfuko wa jimbo pekee haziwezi kusaidia kuleta maendeleo isipokuwa zikichanganywa na za mbunge wa kujiongeza zitakuwa na tija zaidi.

Alisema Kata ya Kalobe ni miongoni mwa maeneo ya Jiji hilo ambayo yamenufaika na michango yake kwa maelezo kuwa katika Shule za Msingi na Sekondari Kalobe alichangia mifuko ya Saruji kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu.

Alisema pia katika Shule ya Sekondari Kalobe alitoa msaada wa komputa pamoja na mashine ya kudurufu maandishi na kwamba endapo atachaguliwa kuwa mbunge atahakikisha barabara inayoelekea kwenye maeneo hayo inaboreshwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Afrey Nsomba, aliwaomba wananchi wa jiji hilo kuwapigia kura wagombea wa chama hicho Oktoba 28 ili kulikomboa Jimbo hilo ambalo kwa muda wa miaka 10 linaongozwa na upinzani.

Aliwataka kuwachagua wagombea wa CCM kuanzia Rais Dk. John Magufuli, Mbunge Dk. Tulia pamoja na madiwani wote wa Chama hicho ili kusiwe na kikwazo wakati wa kuwapelekea maendeleo.

# RUWASA yashauriwa ulinzi miundombinu

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WIZARA ya Maji imeishauri Mamlaka ya Maji mijini na vijijini (RUWASA) wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, kutoa elimu kwa wananchi ili wawe sehemu ya ulinzi wa miundombinu ya maji ambayo inajengwa na Serikali kwa gharama kubwa.

Ushauri huo ulitolewa juzi na mwakilishi wa wizara hiyo, Joash Nyitambe, wakati wa ziara ya maofisa wa wizara hiyo, maofisa wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA) pamoja na maofisa wa RUWASA walipotembelea miradi mbalimbali iliyotekelezwa na serikali wilayani humo.

Nyitambe alitoa ushauri huo baada ya kujionea uharibifu wa miundombinu uliofanywa na wananchi kwenye baadhi ya miradi hasa kukata mabomba na kusababisha maji yasifike maeneo yaliyokusudiwa na serikali.

Moja ya miradi iliyokutwa imeharibiwa ni mradi wa Kanyelele ambao unahudumia wananchi wa Kata ya Mpata wilayani Rungwe ambao mabomba yake yamekatwa na hivyo kusababisha maji yasifikie wananchi.

Alisema kuna uwezekano mkubwa wananchi wanafanya vitendo hivyo kwa sababu hawana elimu ya kutosha kuhusu miradi hiyo na faida zake na pia hawajui madhara ya kufanya uhuni huo.

"Mradi ni mzuri sana na chanzo chake kimewekwa vizuri maana hapa wigo umewekwa vizuri, lakini hili tatizo la wananchi kukata mabomba limenishtua kidogo, niwashauri watu wa RUWASA mje mtowe elimu kwa wananchi juu ya madhara ya wanachokifanya," alisema Nyitambe.

Alisema kitendo cha wananchi kuharibu miundombinu hiyo ni sawa na uhujumu uchumi kwa maelezo kuwa Serikali inawekeza fedha nyingi kwenye utekelezaji wa miradi hiyo na hivyo ikiharibiwa inaigharimu pia serikali fedha nyingi kwenye ukarabati.

Kaimu Meneja RUWASA Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Erastus Kalonga, alisema pamoja na tatizo la uharibifu wa miundombinu ya maji, bado mamlaka hiyo imejitahidi kufikisha maji safi kwa wananchi wa maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo. Alisema mpaka sasa wamefikia zaidi ya asilimia 75 ya upatikanaji wa maji ya bomba katika Wilaya hiyo na kwamba wanaendelea na juhudi za kuhakikisha wanafikia kiwango ambacho kimeainishwa na Serikali.

Alisema Wilaya hiyo ina jumla ya wakazi 428,089 na kwamba kati yao wakazi 318,209 wameshafikiwa na huduma ya majisafi ambayo ni ya bomba tofauti na maeneo mengine ambako huwa yanakuwepo hata maji ya visima.

Alisema Wilaya hiyo ina vyanzo vingi vya maji ambavyo wataendelea kuvitumia kadri watakavyokuwa wanapata fedha ili kuhakikisha wananchi wote wanaanza kupata huduma hiyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mbeya-WSSA, Mhandisi Ndele Mengo, alisema huduma nzuri za maji safi kwa wananchi zinahitaji fedha, lakini kuna baadhi ya wateja wanaochelewa kulipa ama kutolipa kabisa ankara za maji.

Alisema vitendo hivyo vinakwamisha jitihada za Mamlaka katika kutoa huduma bora na kwamba katika kukabiliana na tatizo hilo wanakusudia kuanza kutumia huduma ya malipo ya kabla.



Maofisa kutoka Wizara ya Maji, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) pamoja na wa Mamlaka ya Maji mijini na vijijini (Ruwasa) wa mkoa wa Mbeya, wakikagua moja ya vituo vya kuuzia maji katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mwishoni mwa wiki. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# Ukarabati wa sekondari kongwe wakamilika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema ukarabati wa majengo ya Shule ya Sekondari ya wasichana ya Loleza iliyopo jijini Mbeya na ambayo ni miongoni mwa shule konge nchini, umeshakamilika na wanafunzi wanaendelea na masomo.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu ukarabati wa miundombinu ya shule kongwe na ujenzi wa miundombinu mingine ya elimu katika mkoa huo ambapo alisema ukarabati huo umegharimu Sh. Milioni 899. Alisema kabla shule hiyo haijafanyiwa ukarabati huo, majengo yake yalikuwa na hali mbaya na wanafunzi walikuwa wanasoma kwenye mazingira ambayo hayakuwa salama kutokana na baadhi kuwa katika hatari ya kubomoka.

"Kwa sasa wanafunzi wetu wanaendelea na masomo wakiwa katika hali ya usalama na wana amani ya kutosha, lakini hata wazazi waliowahi kutembelea shule hiyo kwa sasa wana amani kwa sababu sasa watoto wao wanasoma kwenye mazingira salama," alisema Chalamila. Aliishukuru Serikali kwa kuidhinisha fedha hizo pamoja na zilizotumika kukarabati shule zingine Kongwe za Mbeya Sekondari, Iyunga na Rungwe Sekondari kwa maelezo kuwa kwa sasa shule hizo zinapendeza na zinavutia watoto kusoma. Alisema kwa sasa baada ya Serikali kukarabati shule hizo kongwe inaanza mikakati ya kuhakikisha inaimarisha ubora wa taaluma inayotolewa kwenye shule hizo kwa kuhakikisha ufauLu unaongezeka ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vifaa vyote mhimu vinapatikana.

Mbali na ukarabati wa shule hizo kongwe , Chalamila alsema pia mkoa huo ulipokea Sh. Bilioni 4.06 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma ya mabweni, maabara na madarasa kwenye shule mbalimbali mkoani humo.

Alisema fedha hizo zilipokelewa mwishoni mwa mwezi Juni mwaka huu na kwamba zimetumika kukamilisha majengo mbalimbali ya shule 68 za msingi na Sekondari kwenye Halmashauri zote saba za mkoa huo.

Alimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa usimamizi mzuri wa fedha hizo zilizotolewa kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo.



# Majaji, mahakimu watakiwa weledi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAJAJI na mahakimu wametakiwa kufanyakazi kwa weledi kwa kuelewa kila nyanja na kuwa watambuzi wa sheria zitakazowasaidia katika kutoa haki kwa kuwa ndio wanaotegemewa na jamii.

Hayo yalielezwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, katika mafunzo maalum kuhusu taratibu muhimu za sheria za jinai na madai Zanzibar yaliofanyika katika Pemba.

Alisema mahakama ni chombo ambacho kimepewa uwezo wa kisheria wa kusimamia haki, lakini haipaswi kuchelewa, bali itolewe kwa haraka iwezekanavyo.

Alieleza karibu nchi nyingi duniani zinatumia teknojia mpya katika uendeshaji wa kesi mahakamani na kuondokana na uzoefu uliokuwapo nyuma wa kutumia mikono na mashine za kizamani katika uendeshaji wa kesi.

"Katika mabadiliko haya taratibu nyingi ambazo zimeonekana ni kikwazo cha kutenda haki zimeondoka na kuzifanya haki zipatikane kwa haraka sana," alisema Jaji Mkuu.

Alisema miaka ya nyuma katika nchi nyingi kama vile Canada ziliamini majaji wapya hawahitaji mafunzo kwa vile wengi wao wanatoka katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu au mawakili wa kujitegemea kwa vile wana uzoefu wa kimahakama, lakini sasa haiaminiki kutokana na ugumu unaojitokeza wa kuamuwa mashauri mahakamani. Aidha, alisema kutokana na hilo nchi nyingi ulimwenguni majaji wapya hawawezi kuanza kazi kabla ya kupata mafunzo ya vitendo au ya awali.

Hata hivyo alisema kwa vile elimu ni muhimu ndio maana majaji na mahakimu wa Zanzibar wapnapatiwa mafunzo ya muda mfupi ili waweze kujikumbusha taratibu mbalimbali za kisheria.

Alisema ni vyema mafunzo kama hayo yakafanyika kwa watendaji wengine wa ngazi za chini wa mahkama na wadau wengine wa mahkama.

Akitoa mada Jaji mstaafu Mahakama ya Rufani, John Mroso, alisema mafunzo hayo yatawaweka sawa majaji na mahakimu kujiandaa kuhukumu kesi mbalimbali zikiwamo za uchaguzi zitakapojitokeza.

Aliwasisitiza majaji na mahakimu kuzimaliza mapema kesi hizo kama sheria inavyoelekeza, ili kuondoa migogoro kwa wananchi.

Kwa upande wake jaji Fatma Mahmoud alisema mafunzo hayo waliyopatiwa majaji na mahakimu ni muhimu sana kwani yanawaweka utayari katika kuhakikisha wanatoa hukumu stahiki katika kesi



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni (kulia), akimsikiliza Mganga Mkuu wa Hospitali ya Micheweni, Dk.Mbwana Shoka, wakati akitoa taarifa ya maendeleo ya mmoja wa majeruhi wa vurugu za kisiasa zilizotokea Visiwani Pemba, Khatibu Said Khatibu, ambapo alijeruhiwa maeneo ya tumboni na mgongoni kwa kuchomwa kisu na wanaodaiwa wafuasi wa Chama cha ACT Wazalendo. **PICHA :WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

## Zantel yazindua huduma mpya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya simu za mkononi Zantel, imezindua huduma ya Ezy Gazeti ili kurahisisha maisha ya wateja wao kupitia simu za mkononi na kufaidika na huduma zinazotolewa na mtandano huo. Akizungumza katika uziduzi wa huduma hiyo, Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Khamis Mussa, alisema hatua hiyo ni mfululizo wa mikakati ya Zantel katika kuboresha huduma kwa wateja wake. Aidha alisema hatua hiyo pia itatoa suluhisho la kidijitali litakaloziba pengo la upatikanaji wa habari muhimu kwa kuwasaidia watu kusoma magazeti kutumia simu zao za mkononi popote walipo hasa katika maeneo ya vijijini.

Alisema lengo la kuzindua huduma hiyo ni kuwapa fursa wateja kupitia simu zao kuona wanapata magazeti wanayotaka kila siku na kusoma taarifa mbalimbali zinazotokea Tanzania.

"Wengi tumekuwa wateja wa kusoma magazeti yetu na hata pale panaojitokeza taarifa muhimu basi tunakuwa tunayakosa na kukuta magazeti yote yameshamalizika sasa hii ni moja ya kutatua chagamoto ya wateja kuona wanapata gazeti katika mtandano," alisema.

Alisema magazeti pia yanaweza kutumika kupata kumbukumbu za nyuma katika magazeti yake, hivyo hatua hiyo ni muhimu kwa mtandao huo katika kuimarisha maisha ya watu.

Alibainisha kwamba lengo la mtandao huo ni kuhakikisha inatoa huduma mbalimbali ili ziweze kuwarahishia wateja wake. "Zantel tupo kwa ajili ya kutoa huduma siku 365 kwa mwaka na kuona zinawafikia wananchi wote ambao wanatumia mtandao huu," alisema.

Alisema Zantel ipo katika mkakati wa kuona mikopo wa wanafunzi inalipwa kwa kutumia Ezypesa na hata wakulima wa karafuu wanalipwa kwa kutumia huduma hiyo na ZSTC.

Sambamba na hayo, alisema Zantel imejipanga kutoa huduma za kidijital na kuona wateja wote wanakwenda sambamba na mfumo huo.

Hivyo, aliahidi kuwa Zantel itaendelea kurahisisha wateja wake ili kutoa fursa kwa wateja kufanya shughuli nyengine za kimaendeleo.

"Tumeanza na huduma ya kununua umeme, kulipia maji, kununua tiketi za boti na hata leo tumezindua huduma ya Ezy Gazeti kwa kutumia Ezypesa, hii yote ni kuona tunarahisiha maisha ya wateja wote na kunufaika na huduma zetu tunazozitoa," alisema

Naye, Meneja Biashara wa Ezy Gazeti Tanzania kutoka kampuni ya 'Smart Code', Johahhes Julias Lutachalwa, alisema wameungana na Zantel ili kuwa na teknolojia ambayo itaweza kuwarahisishia wateja wao kupata taarifa mbalimbali kiganjani. Alisema hatua hiyo pia itarahisisha watu kupata taarifa mbalimbali ndani na nje ya nchi kupitia magazeti yanayochapishwa Tanzania.

# Shein aeleza umuhimu wa barabara kwa maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema barabara zinafungua milango na kuleta manufaa katika ukuaji na maendeleo ya uchumi na kijamii.

Aliyasema hayo katika ufunguzi wa barabara ya Ole hadi Kengeja yenye urefu wa kilomita 35, katika hafla iliyofanyika katika viwanja vya Shule ya Kengeja, Mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema ujenzi wa barabara unaimarisha makazi ya wananchi na walio wengi huvutika kujenga karibu na maeneo ya barabara ambapo pia shughuli za maendeleo ya biashara, kilimo, uvuvi na nyinginezo nazo huimarika.

"Serikali imejitahidi kuweka mfumo wa barabara katika hali nzuri hivyo, ni wajibu wa Taasisi nyingine zinazohusika na usafiri na usafirishaji pamoja na usalama wa abiria na mizigo kushirikiana pamoja kuona kuwa ajali za barabarani zinapungua."alisema Dk. Shein Aliziagiza mamlaka zinazohusika kuweka alama za usalama barabarani ili ziwaongoze madereva na wapita njia katika kuzitumia barabara vizuri kwa usalama wao na vyombo vya usafiri.

Alisema kujenga barabara ni gharama, lakini ikiwa zitatumika vyema na kupata matunzo mazuri, gharama hizo zinafidiwa na ukuaji wa uchumi kwa mtu mmoja mmoja, jamii na nchi kwa jumla.

"Tumeweza, hatimae tumejenga sisi wenyewe na mkopo wa Benki ya Kimataifa ya Nchi zinazotoa Mafuta kwa wingi (OFID) haukutosha tukaongezea wenyewe, hivyo, wajue kama na sisi wenyewe tuna uwezo mkubwa," alisisitiza.

Aidha, alisema kuwa barabara hiyo ni ya watu wote wa Unguja na Pemba, huku akitumia fursa hiyo kuipongeza Mamlaka ya Mfuko wa barabara (UUB) kwa kutengeneza barabara hiyo pamoja na kuwapongeza viongozi na wafanyakazi wa wizara hiyo.

Rais Dk. Shein alisema njia nyengine ya kuzitunza barabara ni kujiepusha na ajali za barabarani.

Alisema ujenzi wa barabara unagharimu fedha nyingi ambapo kilomita moja inagharimu Sh. bilioni moja kiwango cha lami.

Naye Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alimpongeza Rais Dk. Shein kwa ukamilishaji wa barabara hiyo.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ni sehemu ya jitihada za serikali kuimarisha miundombinu ya barabara kwa lengo la kuimarisha uchumi na maendeleo nchini ambapo pia itaondosha msongamano wa barabara katika mji wa Chake Chake pamoja na kuunganisha Wilaya ya Chake na Mkoani.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mustafa Aboud Jumbe, alisema ujenzi wa barabara hiyo yenye kilomita 35 unajumuisha wilaya mbili za Chake Chake na Mkoani na kupita katika shehia 15.

Pia, alisema barabara hiyo ina upana wa mita 7.5 na imejengwa kwa kiwango cha lami ya moto na ina uwezo wa kutumiwa na gari yenye uzito wa tani 10 ambayo ina madaraja 16.

# Walimu 500 wapatiwa mafunzo ya kidijitali

**Na Christina Mwakangale**

WALIMU zaidi ya 500 wamepatiwa mafunzo ya kidijitali kutoka nchi tofauti ikiwamo Tanzania, ili kuboresha mbinu za ufundishaji darasani.

Mafunzo hayo pia yalitolewa kwa walimu kwenye nchi 80 kwa kipindi cha mwaka jana na mwaka huu.

Balozi wa mafunzo hayo, Josephine Sepeku, akizungumza baada ya mafunzo hayo jijini Dar es Salaam, juzi, alisema kuwa walimu 140 kati ya hao, waliopewa mafunzo mwishoni mwa wiki wamejifunza namna ya kutumia dijitali kwenye ufundishaji.

"Wanafunzi miaka minane hadi 16 kupitia programu ya 'code challenge' tumewaambia waeleze changamoto za kimasomo na kuzitafutia mbinu, mfano masomo ya Hesabu, Fizikia," alisema Josephine.

Alisema mafunzo hayo yanayowezeshwa na Dar Teknohama Business Incubator (DTBI) ni sehemu ya mradi wa 'Africa Codeweek 2020' unaofanyika nchi tofauti.

Pia alisema mafunzo kama hayo yatawafikia wanawake wanaojihusisha na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT), ili kuwaongezea ujuzi.

Doreen Michael, mwalimu wa programu ya 'codeweek' alisema mafunzo hayo yanayotolewa na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), yamelenga kuongeza ushindani wa ajira kwa vijana duniani.

"Mwaka jana tuliwapa mafunzo walimu hao, lengo ni wawe walimu wa kijitali ili wawe bora kuwafundisha wanafunzi ubunifu mbalimbali kupitia teknolojia ya kisasa," alisema Doreen.

Alisema kuwa mafunzo hayo yamewafikia walimu 36,000 na wanafunzi milioni tatu nchi tofauti.

Mshiriki wa mafunzo hayo, Ziredi Juma, ambaye ni Mkurugenzi wa Zerry's Education Centre, alisema mafunzo hayo yamempa mbinu mpya ya ufundishaji watoto.

Alisema yamemjengea uwezo wa kuanzisha programu tofauti ili kumfundisha mwanafunzi kupitia teknolojia ya kidijitali, kumuelewesha awapo darasani.

"Hiki kituo kinachohusika na malezo, mafunzo kwa watoto yaani day care. Tunatumia kompyuta kama tulivyofundishwa, ukifundisha kwa njia ya kawaida darasani, baadhi ya watoto wazito kuelewa, hivyo naweza kutengeneza mfumo wa katuni, ili kuhesabu au kusoma alphabeti," alisema Ziredi.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko Benki ya CRDB, Joseline Kamuhanda, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa kampeni ya "Jipe Tano" inayolenga kuhamasisha wateja kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba. Benki ya CRDB imetenga Sh. Milioni 100 kama zawadi kwa wateja ambao watakuwa wakiweka akiba mara kwa mara katika akaunti zao, ambapo wateja 240 watakuwa wakijishindia fedha kila siku. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni ya kujiwekea akiba yazinduliwa CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imezindua kampeni maalum ya kuhamasisha wateja na Watanzania kwa ujumla kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba iliyopewa jina la "Jipe Tano".

Akizungumza katika uzinduzi huo Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi Benki ya CRDB, Stephen Adili, amesema kampeni hiyo inalenga kuwasaidia wateja kufikia malengo yao ya kimaisha pamoja na kumudu gharama mbalimbali za maisha kupitia utamaduni wa kujiwekea akiba.

"Tunatambua wateja wetu wana malengo ambayo wamejiwekea katika maisha yao, na sisi kama Benki ya kizalendo tuna jukumu la kuhakikisha wateja wetu wanafikia malengo yao kupitia huduma na bidhaa bunifu zinazotolewa na Benki yetu ikiwemo huduma ya kuweka akiba kupitia akaunti mbalimbali," alisema Adili.

Adili alisema katika kampeni hiyo, Benki ya CRDB imetenga kiasi cha Sh. milioni 100 ambapo wateja watakuwa wakijishindia zawadi ya Sh. 5,000 kila watakapokuwa wakiweka akiba katika akaunti zao ikiwamo akaunti ya Watoto Junior Jumbo, Akaunti ya Malkia kwa ajili ya wanawake, Akaunti ya Scholar kwa ajili ya wanafunzi, Akaunti ya Tanzanite kwa ajili ya Watanzania waishio nje ya nchi, akaunti ya pensheni kwa ajili ya wastaafu, Akaunti ya FahariKilimo kwa ajili ya wakulima na akaunti nyingine za uwekezaji kama Thamani, Dhahabu na akaunti za muda maalum.

"Kila mteja atakapokuwa akiweka akiba kwenye akaunti yake atakuwa anapata nafasi ya kujishindia Sh. 5000 kila siku, tunafanya hivi ili kuongeza hamasa kwa wateja kuweka akiba zaidi na kujenga utamaduni huu kwa Watanzania," aliongezea Adili huku akibainisha Benki hiyo itakuwa ikitoa zawadi kwa washindi 240 kila siku hadi mwishoni mwa mwezi Desemba kampeni hiyo itakapofikia kilele.

Akielezea namna ambavyo wateja watakuwa wakijishindia katika kampeni hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Masoko Benki ya CRDB, Joseline Kamuhanda alisema wateja watahitajika kuweka akiba kwenye akaunti zao mara kwa mara ili kushinda zaidi, huku akiwahamasisha wale ambao bado hawana akaunti Benki ya CRDB kufungua na kuanza kujiwekea akiba.

"Kila unapoweka akiba kwenye akaunti yako yoyote iwe kwenye tawi, CRDB Wakala au kupokea salio kupitia SimBanking, Internet banking au kutoka mitandao ya simu na taasisi nyengine za fedha kuingia akaunti yako ya Benki ya CRDB, unajiwekea nafasi ya kushinda shilingi elfu tano kila mara, na ndiomana tunasema Jipe Tano," alisisitiza Kamuhanda.

Kampeni ya Jipe Tano ni mwendelezo wa jitihada za Benki ya CRDB katika kutoa elimu ya huduma za fedha kwa Watanzania, ambapo mapema mwaka huu Benki hiyo iliendesha kampeni ya Popote Inatiki ikihamasisha wateja kutumia mifumo ya kidijitali kupata huduma kwa urahisi na usalama.

# Bosi TRA: Zingatieni sheria mtoze kodi stahiki

**Na Veronica Kazimoto,** DODOMA

NAIBU Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Msafiri Mbibo, amewahimiza watumishi wa mamlaka hiyo kusoma na kuzingatia sheria za kodi ili kuhakikisha wanatoza kodi stahiki.

Akizungumza na watumishi wa Ofisi ya TRA, wilaya za Kondoa na Dodoma Mjini wakati akihitimisha ziara yake mkoani hapa mwishoni mwa wiki, Mbibo alisema ni wajibu wa kila mmoja wao kutenga muda kwa ajili ya kusoma sheria na kuzielewa vizuri ili iwe rahisi kuzitekeleza.

"Kodi haiwezi kukusanywa wala haiwezi kuachwa kukusanywa mpaka pawapo maelekezo ya sheria. Hivyo, usalama wenu katika kukusanya kodi ni lazima msome na kuzingatia sheria zote za kodi zinazosimamiwa na TRA ndipo mtakapoweza kutoza kodi stahiki na kutekeleza majukumu yenu ipasavyo," aliagiza.

Naibu Kamishna Mkuu huyo aliongeza kuwa suala la kujua na kuzingatia sheria za kodi vizuri linaenda sambamba na kuwaelimisha walipakodi kuhusu sheria hizo na siyo kuachia jukumu hilo kwa Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi peke yake.

"Watumishi mlio wengi mnajua kazi ya kuelimisha walipakodi ni jukumu la Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi tu, ninaomba niwaambie kwamba, suala hili ni la kila mtumishi ndani ya TRA na ndiyo maana ninawasisitiza kusoma, kuelewa na kuzingatia sheria vizuri ili kuwaelimisha wateja wetu na hatimaye kuongeza uhiari katika ulipaji kodi," alisema.

Meneja wa TRA Mkoa wa Dodoma, Kabula Mwemezi, alimshukuru Naibu Kamishna Mkuu huyo kwa kufanya ziara katika ofisi zote za TRA mkoani hapa na kuahidi kuendelea kuwasisitiza watumishi kujenga tabia ya kusoma sheria.

Aliahidi kuwa atakikisha watumishi hao wanapewa mafunzo ya mara kwa mara kwa dhumuni la kuwajengea uwezo katika ukusanyaji mapato ya serikali. Pia, alimtembelea Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Suleiman Serera, Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Sezaria Makota na Katibu Tawala wa Wilaya ya Mpwapwa, Sarah Komba.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Conde awania muhula wa tatu urais

**CONAKRY,** Guinea

RAIA wa Guinea wapatao milioni 5.4 walipiga kura jana, huku Rais Alpha Conde akiwania muhula wa tatu wa urais.

Hatua ya Conde ya kuwania muhula mwingine wa urais imesababisha ghasia na chuki miongoni mwa watu wa Guinea. Rais Conde mwenye umri wa miaka 82 amegombea muhula wa tatu baada ya katiba kubadilishwa.

Kwa mujibu wa shirika la haki za binadamu la Amnesty International, takribani watu 50, wengi wao wakiwa wapinzani, waliuawa mnamo mwaka uliopita kwenye maandamano ya kupinga kubadilishwa kwa katiba nchini Guinea. Amnesty International lilisema kufuatia vurugu zilitokea kwa mfululizo katika kipindi cha wiki za hivi karibuni wakati wa kampeni.

**Kufuatia vurugu zilitokea kwa mfululizo katika kipindi cha wiki za hivi karibuni wakati wa kampeni.**

Conde, aliwaambia wafuasi wake katika mkutano wake wa mwisho wa kampeni siku ya Ijumaa uliofanyika kwenye uwanja wa mpira katika mji mkuu, Conakry kwamba mageuzi ya katiba yaliyoidhinishwa katika kura ya maoni Machi, yalikuwa ya haki na ya kidemokrasia.

Alisema anahitaji muda zaidi madarakani kuweza kumaliza mipango mikubwa katika sekta ya madini na miradi ya kuboresha miundombinu.

Guinea imepiga maendeleo katika kukuza utajiri wake wa madini, ambapo pato la taifa hilo limeimarika maradufu chini ya utawala wa rais Conde lakini raia wengi wanalalamika kwamba kuongezeka ufanisi huo katika sekta ya madini bado hakujaleta tija. Ukosefu wa umeme pamoja na ukosefu wa ajira nchini humo bado ni tatizo.

Taifa hilo la Afrika Magharibi limekumbwa na vipindi kadhaa vya machafuko ya kisiasa tangu lilipopata uhuru wake kutoka kwa Ufaransa mwaka 1958, mara nyingi machafuko hayo huchochewa na migogoro ya kikabila. **DW**




Waandamanaji nchini Nigeria kupitia kampeni yao maarufu kama 'Kampeni ya End Sars', wakipinga vitendo vya ukatili vinavyofanywa na Jeshi la Polisi. **PICHA: BBC**

# Utekaji nyara Libya washika kasi

**Tripoli,** Libya

TUME ya Kitaifa ya Haki za Binadamu nchini Libya (NHCR) inalaani kuzuiliwa kiholela kwa mmoja wa wakurugenzi wake ambaye yuko kizuizini tangu Oktoba Mosi, mwaka huu.

Walid Elhouderi anahusika na masuala ya mawasiliano na uratibu wa kimataifa katika Tume hiyo, alichukuliwa na vikosi chini ya amri ya serikali ya umoja wa kitaifa inayoongozwa na Fayez al-Sarraj huko Tripoli.

Kuzuiliwa kwake kiholela kunaangazia tabia sugu inayoendelea nchini Libya.

NHCR inashutumu kuzuiliwa "kimabavu na kiholela" kwa mmoja wa maofisa wake na imetoa wito kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri Mkuu na tume ya Umoja wa Mataifa nchini Libya, kusaidia ili aachiliwe haraka iwezekanavyo. NHCR inainyooshea kidole cha lawama serikali ya Tripoli na kusema ndo itaulizwa kuhusu usalama wake.

Tume hiyo imebaini kwamba maofisa wa idara ya ujasusi ndo walimteka nyara Walid Elhouderi, mtoto wa balozi wa sasa wa Libya nchini Ufaransa na mwanaharakati wa haki za binadamu ambaye RFI imekuwa ikimhoji mara kwa mara.

NHCR inasema "inasikitishwa sana" na dhuluma zote zinazowakumba raia na wanaharakati wa haki za binadamu nchini Libya. Kama raia wengine wengi wa Libya, Walid Elhouderi alitekwa nyara bila waranti, anashikiliwa bila sababu, na hadi Oktoba 1, hajafikishwa mbele ya mwendesha mashitaka mkuu.

Pamoja na wafungwa zaidi ya 1,600waliorekodiwa mwaka 2019, Libya inaongoza kwa orodha nyeusi ya nchi za Afrika kuwazuia watu kiholela na visa vya watu kutoweka kiholela.

Machi, tume ya Umoja wa Mataifa huko Tripoli ilionyesha wasiwasi mkubwa kuhusu hali hii na kuongezeka kwa vitendo vya dhulma dhidi ya raia. **RFI**

## Bensouda anaitembelea Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

UJUMBE wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), utaitembelea Sudan ikiwa ni mara ya kwanza tangu Omar al-Bashir alipoondolewa madarakani mwaka jana, baada ya kufanyika maandamano makubwa yaliyokuwa yakipinga utawala wake.

Ujumbe wa ICC, unapanga kuitembelea Sudan kujadili kesi dhidi ya Rais aliyeondolewa madarakani Omar al-Bashir, na maofisa wengine wa zamani, serikali imesema Jumamosi.

Ujumbe huo unaongozwa na mwendesha mashtaka Fatou Bensouda, utajadili ushirikiano na Sudan juu ya watu wanaotafutwa bila kuwataja majina kulingana na taarifa hiyo.

Ni ziara ya kwanza kufanywa na mahakama hiyo tangu Bashir alipoondolewa madarakani. **VOA**

## Iran: Marufuku ya silaha ya UN imefikia kikomo

**Tehran,** Iran

WIZARA ya mambo ya nje ya Iran, imesema kuwa marufuku ya muda mrefu ya uuzaji silaha kutoka na kuingia nchini humo, imefikia muda wake wa mwisho jana na kuambatana na mkataba wa kihistoria wa nyuklia wa mwaka 2015.

Katika taarifa, wizara hiyo ilisema kuwa kuanzia jana, vikwazo vyote vya kusafirisha silaha, shughuli kuzihusu huduma za kifedha kuingia na kutoka nchini humo vimeondolewa mara moja.

Muda wa marufuku hiyo ya uuzaji wa silaha ulikuwa uanze kufikia kikomo polepole kutokea Jumapili Oktoba 18 chini ya matakwa ya maazimio ya Umoja wa Mataifa yaliofanikisha kubuniwa kwa mkataba huo wa nyuklia kati ya Jamuhuri hiyo ya kiislamu na mataifa yenye ushawishi duniani.

Septemba, mwaka huu, Urusi ilisema kuwa iko tayari kuimarisha ushirikiano wake wa kijeshi na Iran huku China pia ikizungumzia kuwa tayari kuiuzia Iran silaha baada ya Oktoba 18.

Marekani imesisitiza kwamba itatafuta mbinu kuizuia Iran kununua silaha za China na mifumo ya ulinzi wa anga ya Urusi. **DW**

## Uchaguzi wa rais kufanyika Bolivia

**SUCRE,** Bolivia

KARIBU mwaka mmoja baada ya kujiuzulu kwa kiongozi wa zamani wa Kisoshalisti Evo Morales, raia wa Bolivia walipiga kura jana, kumchagua rais wao mpya katika nchi ambayo imegawanyika, ambapo wito umeendelea kutolewa ili kuepusha mgogoro mpya wa kisiasa.

Kwa mara ya kwanza katika miaka 20, Evo Morales (2006-2019), kiongozi wa kihistoria wa mrengo wa kushoto katika kanda ya Amerika Kusini, sio mgombea katika uchaguzi huo.

Novemba 10, mwaka jana, alijiuzulu baada ya Bolivia kutumbukia katika mzozo wa kisiasa, akituhumiwa na upinzani wizi wa kura, wakati alikuwa akiwania muhula wa nne.

Waziri wake wa zamani wa Uchumi, Luis Arce, 57, mgombea kutoka chama cha MAS, na mpinzani wake mkuu, rais wa zamani Carlos Mesa, 67, ndio wanapewa nafasi kubwa ya kushinda katika uchaguzi huo ambao wanachuana wagombea sita.

Kulingana na uchunguzi, Arce, anayechukuliwa kama baba wa "muujiza wa (uchumi) wa Bolivia, anaongoza kwa kura katika duru ya kwanza.

Wabolivia milioni 7.3 wanapiga kura kumchagua rais wao, lakini pia makamu wao wa rais, na kuwachagua wabunge wapya, bunge ambalo kwa sasa linatawaliwa na chama cha MAS.

Kutokana na janga la Corona, kampeni ya uchaguzi ilifanyika kupitia mitandao ya kijamii. **RFI**

# COURTOIS: KIPIGO SASA KIMEIAMSHA MADRID




**MADRID,** Hispania

GOLIKIPA wa Real Madrid, Thibaut Courtois, anaamini kichapo ilichokipata timu yake kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kutoka kwa Cadiz ni kizuri kwani kinawaamsha kuelekea mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na ule wa El Clasico dhidi ya Barcelona.

Bingwa huyo mtetezi alikumbana na kipigo hicho cha kushitukiza cha bao 1-0 kutoka kwa Cadiz, juzi Jumamosi.

Madrid walikubali kichapo hicho kwa bao la Anthony Lozano la dakika ya 16, baada ya lile la Luka Jovic kukataliwa na Karim Benzema aligonga mwamba.

Hicho kilikuwa kipigo cha kwanza kwa Madrid kwa msimu huu wa 2020-21 na kwa mara ya kwanza kutoka kwa Cadiz tangu mwaka 1991, wakati wakijiandaa na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Shakhtar Donetsk na wa Jumamosi wa Clasico pale Camp Nou.

"Kipigo mara zote kizuri kinatuamsha ili tuwe makini na sasa tunatakiwa kuimarika zaidi kwa ajili ya mechi zetu zinazokuja," alisema Courtois baada ya mchezo huo.

"Tunatakiwa sasa kujipanga zaidi, kwani ni wazi kwamba tulionyesha udhaifu hasa kwenye safu yetu ya ulinzi.

"Lakini sasa kuna mechi mbili muhimu zinakuja dhidi ya Shakhtar na ule wa Clasico kule Camp Nou, hivyo tunatakiwa kuwa kwenye morali nzuri zaidi."

# Koeman afura kichapo Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Ronald Koeman, amelalamikia kuhusu "kukosekana kwa heshima" wakati timu yake ikikutana na kichapo kwenye LaLiga kutoka kwa Getafe, huku akimtupia lawama, Allan Nyom.

Koeman alipata kichapo chake cha kwanza kama kocha mpya wa Barca, juzi Jumamosi wakati Getafe wakishinda 1-0 shukrani kwa bao la penalti la Jaime Mata dakika ya 56.

Ulikuwa ushindi wa kwanza kwa Getafe kwenye ligi dhidi ya miamba hao wa Hispania tangu Novemba mwaka 2011.

Koeman, ambaye alirithi mikoba ya Quique Setien mwanzoni mwa msimu huu, alichukizwa na tabia ya mlinzi wa pembeni wa Getafe, Nyom.

"Nilimwambia yeye (kocha wa Getafe, Jose Bordalas) kwamba mchezaji wake namba 12 (Nyom) alionyesha kutokuwa na heshima, alisema mara mbili au mara tatu maneno mabaya sana kwangu mimi na siwezi kurudia. Alinitukana," alisema Koeman baada ya mchezo huo.

"Nilimwambia Bordalas kwamba anatakiwa kuzungumza na mchezaji wake, kwa sababu hatuwezi kuvumilia tabia kama ile kwenye soka la kisasa."

Akijibu kauli ya Koeman, Bordalas alisema: "Nipo hapa kuzungumzia kuhusu soka, si malumbano. Sijazungumza na kijana, nitafanya hivyo kesho, lakini nina shaka kama Nyom anaweza kufanya hivyo, kwa sababu namjua vizuri."





# *Richarlison amwomba msamaha Thiago*

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Everton, Richarlison, ameomba radhi kwa faulo aliyomfanyia Thiago Alcantara kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Liverpool juzi, Jumamosi.

Richarlison alionyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja katika dakika ya 90 wakati timu hizo zikitoka sare ya kufungana mabao 2-2 pale katika dimba la Goodison Park, huku Thiago, akianza kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu tangu ajiunge na klabu hiyo. Kutolewa kwake kulionekana kuigharimu Everton wakati Jordan Henderson alipofunga dakika ya mwisho, kabla ya VAR kulikataa bao hilo kwa kuonyesha kwamba aliotea.

Katika mazungumzo yake baada ya mchezo huo, Jurgen Klopp alibainisha haijulikani Thiago ameumia kwa kiasi gani, lakini anaonekana yuko vizuri.

Richarlison, ambaye aligonga mwamba kwa mpira wake wa kichwa katikati ya kipindi cha pili, aliamua kumuomba radhi Thiago kwa rafu aliyomchezea kwani hakuwa na nia ya kumuumiza.

"Kila mmoja anayejua historia yangu anajua kamwe sikuwahi kuwa mchezaji mwenye fujo," aliandika Richarlison kwenye tovuti yake binafsi.

## HABARI MICHEZO



# MAJERAHA YA VAN DIJK YAMCHANGANYA KLOPP

**LIVERPOOL,** England

KUUMIA goti kwa mlinzi wa Liverpool, Virgil van Dijk si "kitu kizuri", amesema kocha, Jurgen Klopp.

Van Dijk aliumia wakati alipogongana na golikipa wa Everton, Jordan Pickford, katika kipindi cha pili kwenye mchezo wa Ligi Kuu Jumamosi uliomalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Mlinzi huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 29, hakuweza kuendelea na alifanyiwa uchunguzi pamoja na Thiago Alcantara, ambaye pia aliumia goti.

"Virgil amecheza mechi nyingi sana mfululizo na hata sijui idadi yake, anacheza na maumivu, lakini hakuweza kucheza tena," alisema Klopp.

"Hilo si jambo zuri."

Liverpool walitaka penalti kutokana na tukio hilo baada ya Van Dijk kuangushwa, lakini hawakuipata.

"Niliona penalti ya wazi kabisa na tuliona kibendera kilikuwa juu. Nilifikiri wataangalia faulo, lakini hawakufanya chochote," alisema Klopp. "Sitaki kusema kwamba, Jordan Pickford alitaka kufanya vile, lakini ile ilikuwa ni faulo ya wazi kabisa ambayo haifai kufanywa na golikipa."

# Arsenal yamfungua mdomo Guardiola



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anahisi ushindi wa Manchester City wa bao 1-0 dhidi ya Arsenal utasaidia kujenga kujiamini kwa timu hiyo na alitoa sifa kwa safu yake ya ulinzi.

Raheem Sterling alifunga bao pekee kwenye mchezo huo baada ya dakika ya 23 pale kwenye dimba la Etihad, akiuwahi mpira uliomgonga Bernd Leno ambao ulipigwa na Phil Foden. Lakini City pia walionekana kuwa na safu imara ya ushambuliaji tofauti na mechi mbili zilizopita za Ligi Kuu wakati walipofungwa na Leicester City 5-2 na sare ya 1-1 dhidi ya Leeds United.

Kwenye mchezo huo wa Jumamosi, licha ya kumkosa mlinzi wa kati, Aymeric Laporte, kikosi hicho cha Guardiola kiliweza kupata ushindi huo.

Ederson aliokoa hatari kadhaa katika kipindi cha kwanza, huku safu ya ushambuliaji ya Arsenal ikishindwa kuwapita walinzi watatu Kyle Walker, Ruben Dias na Nathan Ake.

"Ulikuwa mchezo mgumu kama tulivyotarajia. Ulikuwa kichwani mwetu, lakini suala la muhimu ni ushindi, hasa kwa matatizo tuliyokuwa nayo," alisema Guardiola akiiambia Sky Sports.

"Kwenye mchezo dhidi ya Leeds, Ederson aliokoa hatari nyingi na amefanya hivyo leo (juzi) dhidi ya Arsenal.

"Kile tulichokifanya leo (juzi), kilikuwa kizuri zaidi na nafikiri Nathan na Ruben walikuwa kwenye kiwango bora kabisa pamoja na Kyle kama mlinzi wa kati".



# *Conte alia na bahati Inter ikichezea mbili*

**MILAN,** Italia

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte, amesema bahati mbaya ndiyo inayopaswa kulaumiwa baada ya timu yake kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa AC Milan, juzi Jumamosi.

Mabao mawili kutoka kwa Zlatan Ibrahimovic yaliwahakikishia ushindi vinara hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, huku Romelu Lukaku akifunga la kufutia machozi kwa Inter.

Inter ilitengeneza nafasi kadhaa za kufunga kwenye mchezo huo, huku VAR ikikataa mabao mawili ya Lukaku baada ya awali kupata penalti.

"Ni bahati mbaya kwamba tumepoteza mchezo. Walikuwa vizuri na nafikiri tulikuwa na bahati mbaya," alisema Conte akiiambia Sky Sport Italia.

"Tulitengeneza nafasi nyingi za kufunga katika kila mchezo. Tunatakiwa kucheza kwa kujituma zaidi, lakini bahati haikuwa upande wetu.

"Lakini siwezi kuwalaumu vijana wangu. Walipambana mwanzo hadi mwisho ili kusawazisha. Lakini hatukuwa na bahati."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: SASA UTD IMEANZA LIGI RASMI

## ●●● Ni wakati wakiichapa Newcastle United 4-1, asema ni matokeo mazuri huku kesho...

**NEWCASTLE,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema Manchester United imeanza rasmi ligi ya msimu wa 2020-21 baada ya juzi, Jumamosi kupata ushindi dhidi ya Newcastle United pale katika dimba la St James' Park.

United ilifumuliwa mabao 6-1 nyumbani na Tottenham katika mchezo wao wa Ligi Kuu uliopita kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa na walionekana kama mambo yangekuwa mabaya tena kwao, baada ya Luke Shaw kujifunga na kuwapa uongozi wa mapema Newcastle katika dakika ya pili.

Hata hivyo, 'Mashetani Wekundu' hao walirudi mchezo na kupata ushindi wa 4-1, huku Harry Maguire akisawazisha na kufuatiwa na mabao ya Bruno Fernandes, Aaron Wan-Bissaka na Marcus Rashford.

**Solskjaer alifurahishwa na ushindi huo na kubainisha kwamba, sasa wao ndio wameanza ligi kwa msimu huu.**

"Ni matokeo mazuri na timu ilionekana kurudi mchezoni haraka, walicheza kwa morali kubwa sana," alisema Solskjaer akinukuliwa na Sky Sports.

"Vijana waliungana vizuri. Na walikuwa makini kwenye mchezo wote. Leo (juzi) niliwapumzisha wachache na walifanya vizuri.

"Harry alifunga na kuongoza kwa mfano. Alionyesha namna gani ni kiongozi mzuri, nina furaha juu yake. Alikuwa na wiki kadhaa ngumu tangu alipotuchezea kwa mara ya mwisho.

"Msimu umeanza leo kwa upande wetu. Tulikuja kwenye mchezo kwa lengo moja tu la kuhakikisha tunashinda na tulifanikisha hilo."

Huku wakikaribiwa na mchezo dhidi ya Paris Saint-Germain kesho Jumanne kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, United tayari itawakosa Anthony Martial na Edinson Cavani.

## ZISIKUPITE

### KOEMAN KUMUONGEZA DEPAY

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman anataka kumuongeza mshambuliaji wa Lyon na Uholanzi, Memphis Depay, mwenye umri wa miaka 26, katika kikosi chake kwenye dirisha la Januari. ***(AD, via Goal)***

### OZIL APEWA MIEZI 2 ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amemuambia Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, kuwa ana miezi miwili tu ya kuthibitisha uwapo wake ndani ya klabu hivyo. ***(Mail)***

### POGBA CHAMBO YA VELVERDE

MANCHESTER United ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Real Madrid na Uruguay, Federico Valverde, mwenye umri wa miaka 22, na inaweza kumtumia, Paul Pogba mwenye miaka 27, katika makubaliano ya mabadilishano. ***(Sun)***

### WIJNALDUM NAYE BARCA

KIUNGO wa kati wa Liverpool na Uholanzi, Georginio Wijnaldum, pia analengwa na Barcelona. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, yuko mwaka wa mwisho wa mkataba wake na msimu ujao atakuwa huru. ***(AD, via Sky Sports)***

### GRACIA ANUKIA BARCA JANUARI

RONALD Koeman ameisihi bodi ya Barcelona kukamilisha uhamisho wa mlinzi wa Manchester City na Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19 wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Mirror)***

### BALE CHUPUCHUPU UNITED

KOCHA wa West Ham, David Moyes, amesema aliandaa helikopta tayari kumchukua juu kwa juu, Gareth Bale aliyetoka Tottenham na kuelekea Real Madrid mwaka 2013, wakati huo akiwa kocha wa Manchester United. Mshambuliaji huyo wa Wales mwenye umri wa miaka 31, hivi karibuni alirejea Spurs kwa mkopo. ***(Mail)***

### RASHFORD AMFURAHIA CAVANI

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 22, amesema kuwasili kwa mshambuliaji wa Uruguay, Edinson Cavani mwenye miaka 33 klabuni hapo, kutaisaidia klabu hiyo kushindania mataji. ***(Sky Sports)***

### JUVE YAMTAJA AOUAR

JUVENTUS ilichagua kumsajili winga wa Italia, Federico Chiesa, mwenye umri wa miaka 22 kutoka Fiorentina, badala ya kiungo wa kati wa Lyon na Ufaransa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22, kipindi cha dirisha la usajili. ***(Sky Sport Italia, via Mail)***

### BOLASIE ALAUMIWA USAJILI

KOCHA wa Middlesbrough, Neil Warnock, amesema Yannick Bolasie mwenye umri wa miaka 31, alistahili kulaumiwa kiasi fulani kwa uhamisho uliofeli kwenye klabu hiyo. Winga huyo alipangiwa kuhamia klabu hiyo kutoka Everton siku ya mwisho ya dirisha la usajili. ***(Teesside Gazette)***

### AFUNGUKA DILI WELBECK

ALIYEKUWA kocha wa Arsenal, Arsene Wenger, amesema alililazimika kuwapiku wapinzani wao Tottenham kumsajili, Danny Welbeck mwenye umri wa miaka 29, kutoka Manchester United mwaka 2014. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

## Mhilu wa Kagera Sugar kama Mugalu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mashabiki wa klabu ya Simba wakimuimba straika wao mpya raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Chris Mugalu, kutokana na kufunga kila anaposhuka dimbani iwe mechi za kirafiki ama za Ligi Kuu, winga wa Kagera Sugar, Yusuph Mhilu ameweka pia rekodi hiyo kwa kucheza mechi tatu na kufunga mfululizo.

Jumatano iliyopita, Mhilu alifunga bao la kufutia machozi kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mjini Lindi, timu yake ikipokea kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya wenyeji Namungo FC na kuwa ni bao lake la nne mfululizo kwenye mechi nne alizocheza.

Mugalu naye amefunga katika mechi zote tatu alizoichezea Simba kwenye Ligi Kuu, lakini Mhilu baada ya kutokuwapo kwenye mechi dhidi ya Yanga Septemba 19 katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba timu yake ikichapwa bao 1-0 ambapo alikuwa majeruhi, mechi yake ya kwanza kucheza ilikuwa Septemba 25 dimba la nyumbani, akifunga bao pekee lililoipa Kagera Sugar ushindi wa bao 1-0.

Akiwa na timu yake jijini Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Azam Complex Oktoba 4, mwaka huu, alifunga bao moja timu yake ikizamishwa mabao 4-2 dhidi ya Azam, kabla ya kufunga tena mechi iliyofuata dhidi ya Namungo.

## Klabu za Soka Zanzibar zafundwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KLABU za soka visiwani Zanzibar zimetakiwa kufuata katiba zao zinazowaongoza hususan katika suala la uchaguzi ili kuwapa fursa wanachama wao kuchagua viongozi ambao watawaletea maendeleo katika timu zao.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Rajab Ali, katika hafla ya harambee ya kuichangia timu ya Jang'ombe Boys inayocheza Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, iliyofanyika juzi usiku katika Ukumbi wa Idrisa Abdul Wakil uliyopo Kikwajuni visiwani hapa.

Mkuu huyo wa wilaya ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, sambamba na kuendesha mchakato huo wa uchangiaji, alisema klabu nyingi hazifuati katiba zao hususan wakati wa uchaguzi jambo ambalo linasababisha kudumaza maendeleo yao kisoka.

# RC MWANZA AZINDUA USAJILI ROCK CITY MARATHON 2020

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amezindua rasmi usajili wa mbio za Rock City Marathon msimu wa 11 huku akitoa wito kwa wadau mbalimbali kutoka Kanda Ziwa kushiriki kikamilifu katika kufanikisha maandalizi ya mbio hizo.

**Mbio hizo zinatarajiwa kufanyika Novemba 29, mwaka huu eneo la Rock City Mall jijini Mwanza.**

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa usajili wa mbio hizo iliyofanyika jana jijini Mwanza, Mongella aliwaomba wadau mbalimbali wakiwamo washiriki na wadhamini kujitokeza kwa wingi ili kuunga mkono mbio hizo zenye agenda ya kutangaza utalii wa ndani katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Katika hafla hiyo ambayo pia ilishuhudiwa na viongozi mbalimbali waandamizi wakijisajili kwa ajili kushiriki katika mbio hizo, Mongella alifunguka: "Nasisitiza ushiriki wa wadau kutoka Kanda ya Ziwa hususan katika Mkoa wa Mwanza kwa sababu hizi ni mbio zetu haitapendeza sana kuona wadau wakuu wa mbio hizi wakiwamo wadhamini na hata washiriki wanatoka kwa wingi mikoa iliyo nje ya Kanda ya Ziwa".

Alitoa wito kwa mashirika na taasisi mbalimbali zikiwamo za watu binafsi kujitokeza ili kuongeza nguvu katika kufanikisha mbio hizo.

Zaidi, Mongella alizipongeza taasisi na mashirika mbalimbali ambayo tayari yamejitokeza kufanikisha mbio hizo ikiwamo Kampuni za TIPER, Pepsi, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Kampuni ya Ujenzi ya CRJE, Pigeon Hotel, CF Hospital, Hospitali ya Bugando, Garda World, The Cask na Chuo cha SAUT Mwanza.

Aidha, aliziagiza halmashauri za Wilaya zote za mkoa huo kupitia maofisa michezo kuhakikisha wanahamasisha usajili wa washiriki wengi iwezekanavyo ili mkoa huo upate wawakilishi wa kutosha kiasi cha kuakisi uenyeji wa mkoa huo katika kuandaa mbio hizo.

"Mkoa wa Mwanza una historia ya kutoa wanariadha wakubwa walioipatia nchi hii heshima katika mchezo wa riadha akiwamo Suleimani Nyambui. Tunahitaji kuendeleza heshima hiyo kupitia mbio hizi hivyo tusimame wote pamoja kufanikisha hili. Washiriki wajitokeze kwa wingi na pia wadhamini wajitokeze kwa wingi," aliongeza.

Katika hafla hiyo, mbali na usajili, Mratibu wa mbio hizo, Kasara Naftal alimkabidhi Mongelle moja ya fulana maalum zitakazotumika katika mbio hizo katika msimu huu huku akibainisha kuwa tayari maandalizi muhimu yameshafanyika ikiwamo suala zima la fulana za washiriki pamoja na medali huku akitaja mbio zitakazohusishwa kuwa ni Km. 21, Km. 10 na Kilomita tano.

Alisema usajili tayari umekwisha anza kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya mbio hizo pamoja na usajili wa kawaida kupitia vituo mbalimbali vilivyopo mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Dodoma, Arusha huku mikoa zaidi ikiendelea kuongezwa.

"Usajili unaendelea vizuri na mwitikio wa washiriki ni mkubwa. Lengo ni kukimbiza washiriki wasiopungua 3000 yakiwamo makundi yote yaani wakimbiaji wa mbio za ushindani (Elite Runners), washiriki wa mbio za kujifurahisha (Fun Run) pamoja na wanafunzi.

"Kuhusu zawadi, pamoja na medali washindi wa kwanza wa mbio za kilomita 21 kwa wanaume na wanawake watajinyakulia Sh. milioni mbili kila mmoja, Sh. milioni 1.3 kwa washindi wa pili na Sh. 700,000 kwa washindi wa tatu, huku washindi wanne hadi kumi nao pia wakiibuka na zawadi za medali na pesa taslimu."




Mratibu wa Mbio za Rock City Marathon, Kasara Naftal (kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, moja ya fulana itakayotumiwa na washiriki wa mbio hizo zitakazofanyika Novemba 29, mwaka huu jijini humo. Katika hafla hiyo ambayo ilikuwa rasmi kwa ajili ya uzinduzi wa usajili, Mongella pia alithibitisha ushiriki wake kwenye mbio za Km. 21. **MPIGAPICHA WETU**

# *Serikali kuwezesha sekta ya michezo nchini*

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa, amesema serikali itaendeelea kuhakikisha sekta ya michezo nchini inawezeshwa ili iweze kuimarika zaidi.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam jana katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, wakati Baraza la Michezo la Taifa (BMT), likiwasilisha mafanikio ya sekta ya michezo kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 - 2020.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kufikia malengo ya nchi katika sekta ya michezo ikijumuisha ujenzi wa miundombinu, upatikanaji wa vifaa vya michezo na kwa bei nzuri, upatikanaji wa wataalamu wa michezo na ubunifu katika kutengeneza vyanzo mbalimbali endelevu vya mapato.

"Ninayaona mafanikio makubwa na bayana ya wanamichezo wetu na timu zetu mbalimbali kutwaa makombe, medali na mikanda. Jambo la kihistoria ambalo halijawahi kutokea hapa nchini, ni la wenzetu wa mpira wa miguu upande wa watu wenye ulemavu kufanikiwa kufuzu kushiriki Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Uingereza," alisema.

Majaliwa alisema mchango wa Sekta ya Michezo katika kujenga umoja, kuimarisha utaifa na maendeleo ya mtu mmoja mmoja, ni mkubwa sana kwani kupitia michezo vijana wetu wanapata ajira, tunatangaza utalii, kuhamasisha kampeni mbalimbali za kijamii, afya, ulinzi na usalama na usafi wa mazingira.

Waziri Mkuu alisema, Serikali chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, inatambua mchango mkubwa wa michezo nchini katika kuleta amani na umoja, kuimarisha afya za wananchi na hivyo kuipunguzia nchi mzigo wa gharama za matibabu, kuchochea utalii, kuendeshea kampeni mbalimbali katika jamii na kutoa ajira kwa vijana.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Leodgar Tenga, alisema ili sekta ya michezo iendelee kuimarika zaidi kunahitajika kuboresha miundombinu na kuwapo kwa vyanzo endelevu vya fedha ambapo kwa sasa vyanzo vikuu vya fedha ni serikali na watu binafsi ambavyo havitoshi.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 19, 2020

Nipashe




Solskjaer: Sasa Utd imeanza ligi rasmi UKURASA 22

DOZI IMEANZA...



Kocha Mkuu wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze, akiwapa dozi ya mazoezi wachezaji wake wakati huu wakijiandaa kuikaribisha Polisi Tanzania katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Alhamisi wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Kaze katika mtihani rekodi ya Krmpotic*

## ●●● Aianzishia Yanga dozi ya kuilewesha Polisi Tanzania kabla ya kuifuata KMC Kirumba, huku akiwa...

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze, tayari ameanza kukipa kikosi chake dozi ya mazoezi wakati huu mashabiki wakitazama namna atakavyoweza kuanza kukiongoza kikosi hicho kwa kulinganisha na rekodi ya kutopoteza mechi yoyote ya mtangulizi wake, Mserbia Zlatko Krmpotic.

**Achilia mbali rekodi ya kutopoteza pia kwenye mechi za kirafiki Krmpotic aliyoiweka Yanga tangu atue wiki moja kabla ya msimu kuanza, lakini pia Mserbia huyo hakupoteza mchezo wowote kati ya mitano ambayo aliiongoza timu hiyo, akishinda minne na kutoka sare moja.**

Hivyo, Kaze ambaye alitua Yanga Alhamisi ya wiki iliyopita, tayari amenza kazi ya kukinoa kikosi hicho ambacho kinashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara kikiwa na alama 13 sawa na Simba iliyopo nafasi ya pili kutokana na kuizidi kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Kaze ambaye ameliambia Nipashe kuwa ana uhakika mashabiki wa timu hiyo watafurahia soka la burudani na ushindani, huku akihitaji muda kuweza kukiunganisha kikosi hicho, kibarua chake cha kwanza kitakuwa dhidi ya Polisi Tanzania katika Uwanja wa Mkapa Alhamisi wiki hii kabla siku tatu baadaye kuifuata KMC FC kwenye dimba la CCM Kirumba jijini Mwanza.

KMC imechagua kutumia Uwanja wa CCM Kirumba kama wake wa nyumbani katika mchezo huo kutokana na kanuni kuruhusu kila klabu kama ikiamua inaweza kucheza mechi mbili nje ya uwanja wake wa nyumbani inaoutumia.

Hata hivyo, Kaze ambaye Oktoba 16 alisaini mkataba wa miaka miwili, tayari ameshaanza kukinoa kikosi cha Yanga kwa ajili ya mechi za ligi ambazo zipo mbele yake akitambua kuwa ipo 'dabi' dhidi ya Simba Novemba 7, mwaka huu inamsubiri.

Yanga itakutana na Polisi Tanzania iliyopo nafasi ya saba baada ya kucheza mechi tano na kujikusanyia alama 10, huo ukiwa ni mtihani wa kwanza kwa Kaze.

Mtangulizi wake Krmpotic mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa Ligi Kuu Bara, yeye alipata sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons kisha kushinda 1-0 dhidi ya Mbeya City mechi zote zikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Baada ya mechi hiyo, Krmpotic akashinda 1-0 ugenini dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba kabla ya kupata ushindi kama huo dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye dimba la Jamhuri, Morogoro na hatimaye kuivurumusha Coastal Union 3-0 Uwanja wa Mkapa.

Hivyo, kwa Kaze baada ya mechi hizo mbili dhidi ya Polisi Tanzania na KMC FC, kibarua pengine kigumu na presha kubwa kitakuwa dhidi ya ya watani zao wa jadi, Simba katika mchezo unaofuata kwenye Uwanja wa Mkapa. Lakini Kaze amesema kikubwa anachohitaji kwa sasa ni sapoti kutoka kwa mashabiki, uongozi pamoja na wachezaji ili aweze kuwapa kile ambacho wanakihitaji ndani ya uwanja.

"Nimfurahia kuwa sehemu ya kikosi chenye mashabiki wengi, ili tuweze kufikia mafanikio ni lazima tupeane sapoti katika kazi. "Natambua mashabiki wanahitaji ushindi, lakini haliwezi kuwa kwa haraka namna hiyo kama wanavyofikiri, ni muhimu kuwa na subira na mambo yatakwenda sawa," alisema kocha huyo ambaye amewahi kufanya kazi katika akademi ya Barcelona.

# Sven achambua makali ya Mugalu

**Na Saada Akida**

HUKU wakiifuata Tanzania Prisons leo kwa ndege hadi Mbeya kabla ya kupanda basi kuifuata mjini Sumbawanga, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck (pichani), amesema amefurahishwa na kasi ya Chris Mugalu ya kucheka na nyavu, lakini pia akieleza atalazimika kubadilisha mfumo kuelekea mechi hiyo itakayochezwa katika Uwanja wa Nelson Mandela, Alhamisi wiki hii.

Mugalu juzi alifunga mabao mawili dakika ya nane na 68 katika ushindi wa 3-1 dhidi ya Mlandege kwenye mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam huku bao lingine likifungwa na Ame Ali dakika ya 16, na la wapinzani Yahya Haji akilitupia dakika ya 72.



Akizungumza na gazeti hili jijini jana, alisema Mugalu ameonyesha kiwango kizuri na ana imani ataisadia timu hiyo kupata idadi ya kubwa ya mabao kwenye mechi za Ligi Kuu. Kuhusu mechi dhidi ya Prisons, Sven alisema mechi za ugenini ni tofauti na wanapocheza nyumbani hali ambayo itamlazimu kuhakikisha anabadili mfumo kulingana na uwanja pamoja na mpinzani wao.

"Mechi ya ugenini kwetu ni ngumu, iwe tunacheza na timu yoyote ile, tofauti na tunapocheza nyumbani, nategemea kubadilisha mfumo kulingana na mpinzani, ila siwezi kuweka wazi juu ya mfumo nitakaotumia.

"Malengo yetu ni kwenda kutafuta ushindi kila mechi ili kufikia malengo, kikosi kipo tayari kwa ajili ya kwenda kutafuta pointi muhimu katika mechi hiyo," alisema Sven ambaye kikosi chake kipo nafasi ya pili kikiwa na alama 13 baada ya michezo mitano.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >